



AUSC
AFRICAN UNION SPORTS COUNCIL

ULINZI KATIKA MAZINGIRA YA MICHEZO NA MICHEZO KWA MAENDELEO (S4D) AFRIKA

Mwongozo wa Watendaji kutoka Sera hadi Vitendo

SHIRIKI KATIKA
KUWALINDA
WATOTO NA
WANAMICHEZO
KATIKA MICHEZO

Published by:
Deutsche Gesellschaft für
Internationale Zusammenarbeit (GIZ) GmbH

Registered offices
Bonn and Eschborn, Germany


Address
Postcode and town, country
T +49 61 96 79-0
F +49 61 96 79-11 15

E info@giz.de
I www.giz.de/en

Author: Regional Project 'Sport for Development in Africa'

Design/layout: Gecko Media Interactive

Nairobi, 2021




DIBAJI

Mwongozo wa watendaji wa Ulinzi katika Michezo umekuja wakati mwafaka ambapo Bara la Afrika linapambana na Janga la COVID-19 huku watoto wakiwa miongoni mwa walioathirika zaidi baada ya mifumo ya elimu kutatizika hivyo kuwa vigumu kwa watoto kushiriki shughuli salama za mazoezi na michezo.

Mwongozo huu muhimu unatoa utaratibu kuhusu jinsi serikali, mashirikisho ya michezo, mashirika, vilabu na watu binafsi wanaofanya kazi katika Spoti na Michezo kwa Maendeleo wanavyoweza kuunda sera, miongozo na kutekeleza hatua zilizoundwa kulinda watoto na watu wazima walio hatarini. Unatoa mchango mkubwa katika kuwalinda watoto kulingana na malengo ya Umoja wa Afrika tunayoitaka yaliyoainishwa katika Ajenda ya 2063 kwa vile azimio la 6 linaisitiza kuwa na "Afrika ambayo maendeleo yake yanaendeshwa na watu, kwa kutegemea uwezo wa watu wa Afrika, hasa wanawake na vijana, na kutunza watoto." Pia unatoa mchango mkubwa katika utekelezaji wa Mkataba wa Afrika wa Haki za Watoto.

Muhimu zaidi, mwongozo huu ni hatua kubwa katika kutimiza mojawapo ya mapendekezo ya mkutano wa kwanza wa kikanda wa mawaziri wa Afrika kuhusu utekelezaji wa Mpango Kazi wa Kazan katika Afrika uliofanyika Antananarivo, Madagaska mwezi Septemba, 2019 ambao ulisisitiza haja ya kuandaa miongozo ya ulinzi na ustawi wa wanamichezo na wadau wengine wa michezo.



MHE Bi. Amira Elfadil

Kamishna wa Afya, Masuala ya Kibinadamu na Maendeleo ya Jamii, wa Tume ya Umoja wa Afrika

Kwa mujibu wa Mkataba wa Baraza la Michezo la Umoja wa Afrika wa 2016 unaohimiza nchi wanachama wote kuunda sera na mikakati zinazofaa za michezo, tungependa kuhimiza Nchi Wanachama na vuguvugu la michezo Afrika kwa ujumla kutumia mwongozo huu ili kuendeleza na kutekeleza sera za ulinzi wa kitaifa hadi ngazi ya chini. Kufanya kipaumbele ulinzi wa kila mtu anayeshiriki katika michezo na shughuli za mazoezi, hasa kwa watoto ni hatua ya kufikia Afrika tunayoitaka.

Hatimaye, tungependa kutoa shukrani zetu kwa Taasisi ya Ushirikiano wa Maendeleo ya Ujerumani kwa kazi kubwa iliyofanywa kuandaa mwongozo huu na tunatarajia ushirikiano huo utaendelea katika jitihada hizi za kutumia michezo ili kuwezesha maendeleo endelevu Afrika.

SHUKRANI

Lengo la 16 la Umoja wa Mataifa la Maendeleo Endelevu linatoa wito wa kukabili aina zote za unyanyasaji na kukomesha dhuluma, ukandamizaji, ulanguzi wa binadamu na aina zote za ukatili na kuteswa kwa watoto. Ingawa washiriki wengi katika michezo wananufaika kutokana na matokeo mazuri kama vile ukuaji wa kimwili na kiakili pamoja na ukuzaji wa stadi za maisha, wengi wao hupitia unyanyasaji na aina nyingine za dhuluma za kimwili.

Ongezeko la uhamasishaji kuhusu hatari za dhuluma za kimwili wakati wa spoti na michezo kwa ajili ya mipango ya maendeleo na umuhimu wa kulinda washiriki linakumbatiwa duniani kote. Michezo na michezo kwa ajili ya miradi ya maendeleo inahitaji kuhakikisha mazingira salama, jumuishi na ya kufurahisha kwa watoto, vijana na watu wazima kufanya mazoezi na kucheza. Kila mtu katika michezo ana jukumu la kuwalinda washiriki. Ulinzi katika Michezo ni wenzu wa watendaji kwa ajili ya mashirika, wawezeshaji - wale wanaofundisha, makocha au wanaoongoza shughuli za michezo, kwa wazazi na walezi na jamii za Afrika. Unatoa mwongozo wa kina kuhusu kuunda sera na desturi

za ulinzi katika spoti na michezo kwa mazingira mbalimbali ya maendeleo na ni wenzu muhimu kwa mafunzo kwa wanariadha, makocha na maafisa wa michezo.

Spoti na Michezo kwa Maendeleo haihusu tu michezo. Shughuli za michezo hutumika kama nyenzo ya kushirikisha watu wanaolengwa katika mipango inayoniua kufikia malengo ya maendeleo kama vile kudumisha amani, usawa wa kijinsia, elimu, umoja na afya. Ili kufanikisha hili, hatua madhubuti za ulinzi ni muhimu katika kuhakikisha haki ya kushiriki katika michezo na shughuli za mazoezi katika mazingira salama na yasiyo na madhara kwa starehe - inatimizwa bila kujali umri, jinsia, asili au uwezo. Mwongozo huu wa watendaji kuhusu Ulinzi katika Mazingira mbalimbali ya Spoti na Michezo kwa Maendeleo (S4D) ni matokeo ya mchakato wa kina na jumuishi ambao uliwahusisha wadau mbalimbali. Umetengenezwa kwa kufuata kanuni bora zinazotambulika, lakini kwa kuzingatia mazingira ya Kiafrika. Umetumia Mifumo ya Kimataifa ya Ulinzi kwa Watoto katika Michezo, Nyenzo za Ulinzi za Kamati ya Kimataifa ya Olimpiki (IOC), Nyenzo za FIFA na mifano mingine ya mbinu bora za ulinzi katika michezo kutoka kote duniani.



Dkt. D. H. Chipande
Mratibu (Mkuu) wa Baraza la Michezo la Umoja wa Afrika

Shukrani za pekee ziende kwa Deutsche Gesellschaft für Internationale Zusammenarbeit (GIZ) GmbH kwa niaba ya Wizara ya Serikali ya Ujerumani ya Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo (BMZ) kwa kutoa usaidizi wa kifedha na kiufundi katika mchakato wa maendeleo. Shukrani nyingi zimwendee Norman Brook - Mtaalamu Mkuu wa Masuala ya Ulinzi katika Michezo (Brook Sport Consulting na mshiriki wa Kikundi Kazi cha Ulinzi wa Kimataifa wa Watoto katika Michezo na Kikundi cha Elimu na Mafunzo cha Safe Sport International), Phil Doorgachurn - Mkurugenzi wa Ulinzi (LimeCulture CIC), Dkt. Lombe Mwambwa - Mkurugenzi Mtendaji, (Shirika la Kitaifa la Wanawake katika Michezo, Shughuli za Mazoezi na Burudani, Zambia), Liz Twyford - Mtaalamu wa Miradi ya Michezo, Unicef Uingereza.

Mwisho, ningependa kutambua juhudi za wadau wengine ambao labda hawakutajwa hapa kwa mchango wao muhimu wakati wa kuandaa mwongozo huu.



UTANGULIZI

Michezo na shughuli za mazoezi zinatambuliwa kimataifa kuwa nyenzo muhimu ya kuwezesha maendeleo endelevu. Inakuza ukuaji wa kijumla kwa watoto na vijana, bila kujali umri wao, jinsia, asili, mienendo ya kijinsia, au kama wana ulemavu wowote au mahitaji maalum. Michezo na shughuli za mazoezi huchangia ukuaji wa watu kijamii, kiakili na kimwili, na kukuza jamii zenye afya na ushirikiano wa karibu.

Hata hivyo, ni muhimu zaidi kuhakikisha michezo inasaidia maendeleo kamilifu ya watoto na vijana na kwamba haiathiri vibaya haki zao (Haki za Watoto katika Kanuni za Michezo, UNICEF 2018,). Mwongozo wa Ulinzi unahusu hatua zinazochukuliwa ili kukuza usitawi wa watoto, vijana na watu wazima walio katika mazingira hatari ili kuhakikisha kuwa wanakuwa salama, bila madhara. Unajumuisha kufanya kila linalowezekana ili kupunguza hatari zinazopatikana katika mazingira haya na kuzuia aina zote za unyanyasaji, dhuluma, kutelekezwa au kukandamizwa huku tukihakikisha kwamba watoto, vijana na watu wazima wanaweza kushiriki katika michezo katika mazingira salama ambayo yanakuza starehe. Kulinda pia kunahusu kushughulikia ipasavyo masuala yanayotolewa kuhusu watoto, vijana au watu wazima wanaokabiliwa na hatari ya kuathirika vibaya.


Mwongozo huu wa Ulinzi katika Michezo unatoa utaratibu kwa serikali, mashirika, taasisi, mashirikisho na watu binafsi wanaofanya kazi katika spoti na Michezo kwa Maendeleo kuhusu kuandaa sera,

miongozo na utekelezaji wa hatua inayoundwa kulinda watoto na watu wazima dhidi ya maumivu yasiyo ya kijajali. Ingawa sehemu kubwa ya mwongozo huu inahusika na kuwalinda watoto na vijana kwa sababu wako katika hatari kubwa ya kudhulumiwa na kutumiwa vibaya, iwe kwa kupendelea au la, tunatambua kuwa njia bora zaidi ni kuwalinda watoto na watu wazima wote wanaohusishwa na aina yoyote ya shughuli za Spoti na Michezo kwa Maendeleo.

Pia tunatambua kwamba shughuli za Michezo kwa Maendeleo huwa katika mazingira yenye changamoto, ambapo watoto na watu wazima wanaweza kuwa katika hatari kubwa ya madhara kwa sababu tu ya mazingira wanayoishi.

Mwongozo huu unatambuliza dhana ya ulinzi na kuangazia desturi bora ni zipi katika suala la michezo au shirika la Michezo kwa Maendeleo, wale wanaotoa mafunzo (wawezeshaji) na jinsi washiriki wa miradi wanaweza kushiriki kwenye ulinzi katika ngazi ya kijamii.

Mchoro wa 1: Yaliyomo katika Mwongozo huu yamepangwa kutegemea shirika, wawezeshaji na jamii inayohudumiwa.



Kuwa na **mwendelezo**, tumewaita wanaotoa mafunzo ya Spoti na Michezo kwa Maendeleo, walimu, makocha, washauri, viongozi wa rika, n.k. wawe ni wafanyakazi au watu wa kujitolea; **wawezeshaji**. Pia tumewataja wale wanaoshiriki katika shughuli za spoti au Michezo kwa Maendeleo kuwa ni **washiriki**, tukitambua kwamba wengi watakuwa watoto na vijana, lakini wengine watakuwa watu wazima.



FASILI

UONEVU NADHULUMAZAKIMTANDAO hutokea wakati mtu (au watu) wanapolenga kumdhuru, kumtisha au kumlazimisha mtu anayechukuliwa kuwa ni myonge, iwe ni ana kwa ana (uonevu) au mtandaoni (unyanyasaji wa mtandaoni). Uonevu unaweza kuhusisha vitendo vinavyorudiwa na vya makusudi au tabia ya kuumiza ambayo hurudiwa kila wakati.

WATOTO hufafanuliwa kuwa ni vijana walio chini ya umri wa miaka 18. Wanalindwa chini ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Watoto, ambao umepitishwa na mataifa 197.

DHULUMA ZA KINYUMBANI inamaanisha tukio au matukio ya kudhibiti, kulazimisha, vitisho, udhalilishaji na tabia ya ukatili, ikiwa ni pamoja na unyanyasaji wa kijinsia, katika matukio mengi yanayofanywa na mpenzi au mpenzi wa zamani, lakini pia na mwanafamilia au mlezi. Dhuluma za kinyumbani hutokea sana, na, mara nyingi, hutokea kwa wanawake na hufanywa na wanaume. Dhuluma za Kinyumbani zinaweza kujumuisha, lakini si tu, unyanyasaji kati ya wapenzi (IPV), udhibiti wa kulazimishwa (mfano wa vitisho, udhalilishaji, kutengwa na udhibiti kwa kutumia au kutishia unyanyasaji wa kimwili au wa kingono), unyanyasaji wa kisaikolojia / kihisia, unyanyasaji wa kingono, unyanyasaji wa kifedha au kiuchumi, uchokozi na kuvizia, na unyanyasaji wa mtandaoni au dijitali.

Mtoto kushuhudia dhuluma za kinyumbani au unyanyasaji kati ya wapenzi, ni hali inayochukuliwa kuwa aina ya unyanyasaji wa kisaikolojia au kihisia kwa mtoto.

UDHALILISHAJI ni kitendo cha ubinafsi cha kumtendea mtu au kikundi cha watu ili kufaidika kutoka nao au kujinufaisha kwa namna nyingine.

MWEZESHAJI ni mtu yeyote ambaye hutoa elimu ya viungo vya mwili, mazoezi, michezo au shughuli za Michezo kwa Maendeleo kwa washiriki ambapo wanaweza kuwa walimu, makocha, washauri, viongozi rika, n.k.

UNYANYASAJI WA KIFEDHA uinahusu matumizi mabaya ya rasilimali za kifedha au matumizi mabaya ya udhibiti wa kifedha katika uhusiano ambao unategemea kuwapo kwa uaminifu. Watu wazima walio katika hatari, wanawake walio katika mahusiano mabaya na watu walio wazidi umri wanaweza kuwa katika hatari ya kunyanyaswa kifedha. Unyanyasaji wa kifedha wakati mwingine unaweza kukosa kuonekana ama kuwa vigumu kutambua na mara nyingi huhusishwa na aina nyingine za dhuluma.

Mifano ni kama vile:

- Mtu kuchukua au kutumia vibaya pesa au vitu vya mtu mwingine kwa faida yake binafsi.
- Kudhuru, kunyima au kudhoofisha mtu kwa kumnyima ufikiaji wa rasilimali.
- Kudhibiti ununuzi wa mtu mwingine au uwezo wake wa kufikia pesa.
- Tabia ya unyanyasaji wa kifedha ambayo mara nyingi si uhalifu kama vile wizi au ulaghai.

URAFIKI WA KUPUMBAZANI ni kitendo cha kufanya urafiki na kuanzisha uhusiano wa kihisia na mtoto, kijana au mtu mzima aliye katika mazingira hatari, na wakati mwingine familia zao, kwa njama ya kuwashawishi kwa lengo la kutekeleza udhalilishaji au unyanyasaji wa kingono. Urafiki wa kupumbaza unaweza kufanyika mtandaoni au kwa mazungumzo au moja kwa moja kati ya watu wasiojuana au wanaojuana – mwanafamilia, rafiki au mtaalamu.

ITIKADI KALI inahusu sherehe za jandoni, ikiwa ni pamoja na matambiko, mashindano na shughuli nyinginezo, zinazohusisha unyanyasaji, kudhulumu au udhalilishaji kama njia ya kuingiza mtu katika kikundi, kama vile timu ya michezo.

UNYANYASAJI hufafanuliwa kuwa vitendo visivyokubalika vya dharau ambapo hujumuisha vitisho vya maneno au vitu vya kuudhi. Mtu yeyote anafaa kuamua kile anachokiona kuwa kinakubalika na kile anachokiona kuwa cha kuudhi.

KUTELEKEZWA ni hali ya kushindwa kushughulikia mtoto au mahitaji ya kimsingi ya watu wazima katika mazingira hatari, kama vile kuwaacha wakiwa na njaa au wachafu, bila mavazi, makao, uangalizi au huduma za afya zinazofaa.

MATUSI MTANDAONI ni aina yoyote ya unyanyasaji unaotokea kwenye mtandao. Unaweza kutokea kwenye kifaa chochote ambacho kimeunganishwa kwenye wavuti, kama vile kompyuta, kipakatalishi au simu za mkononi. Matusi ya mtandaoni yanaweza kutokea popote kwenye mtandao, kupitia:

- mitandao ya kijamii
- SMS na programu za kutuma ujumbe
- barua pepe
- gumzo mtandaoni
- michezo ya mtandaoni
- tovuti za matangazo mbashara

Watoto na watu wazima wanaweza kuwa katika hatari ya kunyanyaswa mtandaoni na watu wanaowajua au wasiowafahamu. Huenda ikawa sehemu ya unyanyasaji mwingine unaofanyika nje ya mtandao, kama vile urafiki wa kupumbaza, au unyanyasaji unaweza kutokea mtandaoni pekee.

MASHIRIKA inamaanisha shirika lolote ambalo lina miradi ya Spoti au Michezo kwa Maendeleo. Yanaweza kuwa ya kiserikali, yasiyo za kiserikali au ya kijamii, na yaliyopo katika ngazi ya kitaifa, kikanda au kimataifa.

WASHIRIKI inamaanisha walengwa wa miradi ya spoti na Michezo kwa Maendeleo. Washiriki kwa kawaida ni watoto au vijana lakini wanaweza kujumuisha watu wazima.

WATU WENYE MATATIZO YA KIAKILI inamaanisha watoto walio chini ya umri wa miaka 18 au watu wazima zaidi ya umri wa miaka 18 ambao wanahitaji, au wanaweza kuhitaji huduma kwa sababu za ulemavu wa kiakili.

MTU MWENYE ULEMAVU WA MWILI inamaanisha watoto chini ya umri wa miaka 18 au watu wazima zaidi ya miaka 18 ambao wanahitaji huduma kwa sababu ya ulemavu wa kimwili.

UNYANYASAJI WA KIMWILI inahusu dhuluma yoyote ya makusudi na kitendo kisichokubalika – kama vile, kupiga ngumi, kuchapa, kupiga teke, kuuma na kuchoma – ambacho husababisha maumivu ya kimwili au majeraha. Vitendo kama hivyo vinaweza pia kuwa vya kulazimishwa au mazoezi yasiyofaa kwa mwili (kwa mfano, mafunzo yanayozidi umri au uwezo wa mwili; shughuli za kushurutishwa wakati mtu amejeruhiwa au akiwa na maumivu), kulazimishwa kunywaji pombe au kulazimishwa kutumia dawa za kususimua misuli.

UNYANYASAJI WA KISAIKOLOJIA (KIHISIA AU KIAKILI) Unahusu tendo lolote lisilokubalika, ikiwa ni pamoja na kifungo, kutengwa, kutusiwa, kudhalilisha, vitisho, kufanywa mtoto mchanga au mateso mengine ambayo yanaweza kupunguza

hisia ya kujitambua, kujiheshimu na kujithamini. Unyanyasaji wa kisaikolojia ni aina yoyote ya dhuluma inayohusisha unyanyasaji wa kila mara wa kihisia kwa mtoto au mtu mzima. Unaweza kuhusisha jaribio la kutisha kimakusudi, kufedhehesha, kutenga au kupuuzwa mtoto au mtu mzima.

Unyanyasaji wa kisaikolojia au kihisia mara nyingi hutokea kutokana na aina nyingine za unyanyasaji, ingawa unaweza pia kutokea peke yake.

MAWASILIANO YA MARA KWA MARA inafanuliwa kuwa mawasiliano ya kufanyika zaidi ya mara moja kwa mwezi.

DHULUMA ZA KINGONO inafanuliwa kuwa mwenendo wowote wa kingono, uwe usio wa kimwili, kugusana au kujamiihana, ambao unalazimishwa/kutumiwa au kufanywa bila idhini kutolewa au hauwezi kutolewa.

UDHALILISHAJI WA KINGONO unahusu tendo halisi au jaribio la kutumia vibaya mamlaka au uaminifu kwa madhumuni ya ngono, kwa mtu ambaye yuko katika hatari, kwa lengo la kunufaika kifedha, kijamii au kisiasa kutokana na kumkandamiza mtu mwingine kingono.

UNYANYASAJI WA KIJINSIA ni tendo lolote lisilotakikana na tabia isiyokubalika ya kingono, iwe kwa maneno, au matendo ya kimwili. Unyanyasaji wa kijinsia unaweza kuchukua mkondo wa dhuluma za kingono.

ULANGUZI WA BINADAMU ni mchakato wa kuajiri, kuhamisha au kusafirisha wanawake, wanaume au watoto kwa sababu ya kuwadhulumu, kwa kuwapa kazi ya kulazimishwa ama kuwauza.

Mara nyingi wao huhamishwa mbali na nyumbani kwao na kulazimishwa kufanya kazi katika biashara ya ngono. Ulanguzi wa binadamu unaweza kuhusisha matumizi ya nguvu, ulaghai au kulazimisha na kusababisha utumwa wa kisasa, ambao ni ukandamizaji sugu wa watu kwa faida ya kibinafsi au ya kibiashara.

WATU WALIO KWENYE HATARI ni mtu yeyote mwenye umri wa miaka 18 ama zaidi, au anayeweza kuhitaji huduma kwa sababu ya ulemavu, umri au pengine ugonjwa, au anaweza kuwa, hawezi kujihudumia mwenyewe. Inajumuisha mtu yeyote mwenye umri wa zaidi ya miaka 18 ambaye hawezi kujilinda dhidi ya unyanyasaji, dhuluma, kutelekezwa au ukandamizaji kutokana na uwezo wake wa kimwili, rangi, jinsia, ujauzito, kuoa/kuoleka, kabila au asili ya kijamii, mwelekeo wa kijinsia, umri, ulemavu, dini, mawazo, imani, utamaduni, lugha au kuzaliwa. Katika mazingira ya Afrika, ambapo kuna viwango vya juu vya ukatili wa kijinsia, baadhi ya wanawake wanaweza kuchukuliwa kuwa hatarini. Makundi mengine ambayo yanaweza kuwa katika hatari kwenye mazingira ya Kiafrika ni pamoja na kundi la LGBTQIAP+ watu waliotengwa kutokana na utambulisho wa jinsia tata, wakimbizi na watu waliokimbia makazi yao (IDP), pamoja na watu wanaoishi na VVU na UKIMWI.

VIJANA wanatambuliwa kuwa watu wenye umri kati ya miaka 15 na 24 ambao wanakua kutoka utotoni hadi utu uzima. Kwa uzoefu mdogo wa maisha bado hawajapata ustahimilivu na wanaweza kuwa katika hatari zaidi ya kukandamizwa, kudhulumiwa au kunyanyaswa. Vijana walio chini ya umri wa miaka 18 wanatambuliwa kuwa watoto na wanalindwa chini ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Watoto na sheria za kitaifa.

KUELEWA ULINZI

Ulinzi katika mazingira ya Spoti na Michezo kwa Maendeleo ni jukumu la taasisi na mashirika, ambayo lazima yahakikishe wafanyakazi wao, watu wanaojitolea, shughuli zao, na miradi yao haidhuru watoto, vijana au watu wazima walio katika mazingira hatari, au kuwaweka kwenye unyanyasaji, dhuluma, kutelekezwa au ukandamizaji. Taasisi na mashirika haya lazima yahakikishe yana mifumo ifaayo ili kushughulikia masuala mbalimbali.

Ingawa mashirika mengi ya Spoti na Michezo kwa Maendeleo yanazingatia kuwalinda watoto, inazidi kuwa desturi bora kuzingatia jinsi tunavyoweza kulinda kila mtu anayeguswa na miradi yetu, wakiwamo wafanyakazi, watu wanaojitolea na wanajamii, kwa kuwalinda dhidi ya tabia zisizofaa kama vile uonevu na unyanyasaji.

Hatua za ulinzi zinalenga kulinda afya, ustawi na haki za binadamu za watu binafsi, hivyo kuruhusu watu, hasa watoto, vijana na watu wazima walio katika mazingira hatari, kuishi bila madhara, huku wakikuza haki yao ya kushiriki michezo katika mazingira salama na ya kufurahisha. Haki za binadamu kwa watu binafsi zimewekwa katika Azimio la Umoja wa Mataifa la Haki za Kibinadamu, hasa kwa watoto, katika Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Watoto. Haki hizi mara nyingi hujumuishwa katika katiba za kitaifa kupitia sheria au sera maalum za kitaifa na mifumo ya kisheria.

Ulinzi wa mtoto ni sehemu ya mchakato wa ulinzi na unarejelea hatua zinazowalinda watoto ambao wametambuliwa kuwa wanaoteseka au wanaoweza kupata madhara makubwa. Ulinzi unajumuisha sera na shughuli ambazo mashirika ya spoti na Michezo kwa Maendeleo hufanya ili kuwaweka watoto salama, kukuza ukuaji wao na kushughulikia maslahi yao.

Miradi ya Spoti na Michezo kwa Maendeleo inahitaji sera na hatua madhubuti za ulinzi kama vile:

- Michezo inatambulika kuwa ni shughuli ya kustarehesha/ mazoezi ya mwili na ujuzi ambayo mara nyingi huwa wa ushindani ambapo watoto, vijana na watu wazima walio katika mazingira hatari wanaweza kukumbana na unyanyasaji, dhuluma, kupuuzwa au ukandamizwa.
- Miradi ya Michezo kwa Maendeleo (S4D), ambayo inahusisha matumizi ya mazoezi ya kimwili, elimu ya viungo, spoti, mchezo, burudani, kucheza ngoma na michezo ya kitamaduni ili kukuza maendeleo ya kijamii na kiuchumi kupitia mafunzo ya uzoefu, hufanyika pale ambapo masuala ya kijamii yanayojenga mazingira ambayo huwaweka washiriki katika hatari zaidi ya kunyanyaswa, kudhulumiwa, kutelekezwa au ukandamizwa katika jamii yao.

Ukuaji mzuri wa watoto unachukuliwa kuwa wa muhimu sana na nchi nyingi zina sheria ya kuwalinda watoto, ikijumuisha hitaji la lazima la kwa polisi au shirika la huduma za kijamii. Kuwalinda watoto ni jukumu la kila mtu.

Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Watoto unajumuisha haki mbalimbali, kama vile:

- Watoto wana haki yao ya kutoa maoni, na kwa watu wazima kusikiliza na kuchukua maoni hayo kwa uzito (Kifungu cha 12).
- Watoto wana haki ya kulindwa dhidi ya kuumizwa na dhidi ya unyanyasaji wa kiakili na kimwili kuripoti aina mbaya za unyanyasaji wa kimwili miongoni mwa watoto (Kifungu cha 19).
- Watoto wana haki ya kucheza na kupumzika (Kifungu cha 31).
- Watoto wana haki ya kuwa huru dhidi ya udhalilishaji wa kingono na kiuchumi (Kifungu cha 34).

Kuna wajibu kwa mashirika kuhakikisha washiriki wote, watoto na watu wazima, wanaweza kushiriki katika miradi ya michezo na S4D ambayo ni salama, iliyo jumuiishi na inayofurahisha. Washiriki wanapaswa kuwa na uwezo wa kushiriki katika shughuli kwenye mazingira yasiyo na madhara, bila kujali rangi, jinsia, ujuzito, kuo/kuoleka, kabila au asili ya kijamii, mwelekeo wa kijinsia, umri, maumbile, dini, mawazo, imani, utamaduni, lugha, na kuzaliwa au uwezo wa kiriadha.

Mtu yeyote anaweza kupata madhara, lakini tunajua kwamba baadhi ya vikundi vinaweza kuathiriwa hasa kutokana na sababu mbalimbali.

Jedwali la 1: Mifano ya makundi ya watu ambao wanaweza kuathirika zaidi katika mazingira ya michezo.

Watoto na vijana	Wanajamii wa LGBTQIAP+
Vijana	Wakimbizi na wakimbizi wa ndani kwa ndani (IDP)
Wanariadha wenye vipaji	Jamii ndogondogo nchini
Watu wenye tatizo la afya ya akili	Watu wa asili
Watu wenye matatizo ya kiakili	Wazee
Watu wenye ulemavu wa kimwili	Watu wanaoishi na VVU na UKIMWI
Wanawake na wasichana	Watu wanaoishi katika umaskini

Mwenendo Usiokubalika

Kuna viwango tofauti vya maadili vinavyotarajiwa kutoka kwa mtu yeyote anayehusishwa na spoti au Michezo kwa Maendeleo ambavyo vitahitaji kushughulikiwa.

1. Mwenendo ambao ni kinyume na sheria utahitajika kuripotiwa kwa mamlaka ili kushughulikiwa.
2. Mienendo ambayo inaathiri kanuni za maadili ya shirika na inaweza kusababisha mfanyakazi kufukuzwa kazi au hatua nyingine za kinidhamu.
3. Mwenendo wa utendakazi duni na ambao utahitaji kushughulikiwa kupitia mchakato wa kukagua utendakazi.

Mwenendo unaohusishwa na unyanyasaji, dhuluma, kutelekezwa au ukandamizaji ni mbaya kiasi cha kutakiwa kuripoti kwa mamlaka. Katika matukio yanayowahusu watoto, hitaji la lazima kuripoti

linaweza kuwa katika sheria. Mwenendo mwingine ambao unaweza kuzingatiwa kuwa ukiukaji wa kanuni za maadili ya shirika na zinahitaji kuwekewa baadhi ya vikwazo. Baadhi ya mienendo inaweza kukosa kukiuka kanuni za maadili lakini inaweza kuchukuliwa kuwa utendakazi mbaya kwa hivyo inahitaji kushughulikiwa na mtu anayehusika. Utendakazi duni unafaa kushughulikiwa kwani kushindwa kufanya hivyo kunaweza kuleta mienendo ambayo itawadhuru washiriki ndani ya shirika.

Aina za Dhuluma

Kuna aina nne za dhuluma zinazotambuliwa na Shirika la Afya Duniani (WHO), UNICEF na Vituo vya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa (CDC): kimwili, kisaikolojia (kihisia au kiakili), kingono na kutelekezwa.

Zimefafanuliwa hapa chini, zikiambatana na mifano ya matukio hatari ya unyanyasaji ambayo yanafaa

kuripotiwa kwa mamlaka, kisa kibaya zaidi kinapaswa kushughulikiwa kupitia taratibu za kinidhamu za shirika lenyewe na kisa kisichokuwa kibaya zaidi ambacho kinajumuisha utendakazi duni ambao unapaswa kushughulikiwa kupitia ukaguzi wa utendaji.

Unyanyasaji wa Kimwili

Unyanyasaji wa kimwili unahusu dhuluma yoyote ya makusudi na kitendo kisichokubalika – kama vile, kupiga ngumi, kuchapa, kupiga teke, kuuma na kuchoma – ambacho husababisha maumivu ya kimwili au majeraha. Vitendo kama hivyo vinaweza pia kuwa vya kulazimishwa au mazoezi yasiyofaa kwa mwili (kwa mfano, mafunzo yanayozidi umri au uwezo wa mwili; shughuli za kushurutishwa wakati mtu amejeruhiwa au akiwa na maumivu), kulazimishwa kunywaji pombe au kulazimishwa kutumia dawa za kusisimua misuli.

Mwezeshaji kumpiga mshiriki ngumi kichwani mara kadhaa kwa kukosa bao wakati wa mechi.	Kosa la Jinai¹
Mwezeshaji kuwafanya watoto kulia mara kwa mara kwa kuwapa mazoezi ambayo hayaendani na umri.	Mienendo ya Kinidhamu
Mwezeshaji huwafanya watoto kukimbia mizunguko ya uwanja wa michezo kama adhabu kwa kushindwa jukumu.	Tathmini ya Utendakazi

Unyanyasaji wa Kisaikolojia

Unyanyasaji wa kisaikolojia (kihisia au kiakili) ni kitendo chochote kisichokubalika, kama vile kufungwa, kutengwa, kushambuliwa kwa maneno, udhalilishaji, vitisho, kufanywa kama watoto wachanga au mateso mengine yoyote, ambayo yanaweza kushusha hadhi ya mtu, heshima na kujithamini.

Katika hali ambapo mtu anakabiliwa na unyanyasaji wa kimwili, dhuluma za kijinsia au kutelekezwa, wao pia wanakabiliwa na unyanyasaji wa kisaikolojia.

Mwezeshaji anaanza kutuma ujumbe wa kibinafsi ambao haufai au anaanza njama ya kumfuatilia mshiriki.	Mienendo ya Kihalifu
Mwezeshaji mara kwa mara humcheka mshiriki na kuwahimiza washiriki wengine kucheka wakati mshiriki anapofanya makosa.	Mienendo ya Kinidhamu
Mwezeshaji anaonesha upendeleo katika timu na matokeo yakiwa ni kwamba baadhi ya washiriki wanahisi kutengwa.	Tathmini ya Utendakazi

Unyanyasaji wa Kingono

Unyanyasaji wa kingono unarejelea tabia yoyote ya asili ya ngono, iwe isiyo ya kimwili, kugusana au kujamiiana, kwa kulazimishwa/kutumiwa au kufanywa bila idhini kutolewa au haiwezi kutolewa.

Mwezeshaji anambaka au kumnajisi mshiriki.	Mienendo ya Kihalifu
Mwezeshaji anasisitiza kwa washiriki kuvaav mavazi yanayoonesha maumbile wakati wa kufanya mazoezi.	Mienendo ya Kinidhamu
Mwezeshaji anapendelea wanariadha wa kike kuliko wanariadha wa kiume au kinyume chake.	Tathmini ya Utendakazi

Kutelekezwa

Kutelekeza kunamaanisha mwezeshaji au mtu mwingine aliye na jukumu la kumtunza mshiriki kushindwa kushughulikia maslahi ya mtu, hivyo kusababisha madhara, kuruhusu madhara kutokea au kumweka mtu huyo katika hatari.

Mwezeshaji anawapeleka washiriki kuogelea bila mikakati wala vifaa vya kutosha vya usalama kisha mshiriki anazama.	Mienendo ya Kihalifu
Mwezeshaji anashindwa kuweka rekodi ya mahudhurio kisha mtoto anapotea kwenye kipindi bila kutambuliwa.	Mienendo ya Kinidhamu
Mwezeshaji kukosa kupanga muda wa mapumziko ya kunywa maji wakati wa mazoezi katika joto. ²	Tathmini ya Utendakazi

¹ Ikiwa tukio la kutelekezwa, unyanyasaji wa kimwili, kisaikolojia au kijinsia litachukuliwa kuwa mwenendo wa uhalifu basi itategemea sheria katika nchi ambako madai ya unyanyasaji yalifanyika.
² Utendakazi duni mara nyingi unaweza kuongezeka kwa haraka kiasi cha kutaka kuripotiwa au kushughulikiwa kupitia michakato ya kinidhamu.

Mienendo ya Kuleta Madhara

Ingawa aina nyingi za madhara zinahusisha aina moja au zaidi za unyanyasaji, kuna aina nyingine mahususi ya mienendo inazosababisha madhara ambayo inastahili kuzingatiwa.

Unyanyasaji

Unyanyasaji hufafanuliwa kuwa vitendo visivyokubalika vya dharau ambapo hujumuisha vitisho vya maneno au vitu vya kuudhi. Mtu yeyote anafaa kuamua kile anachokiona kuwa cha kukubalika na kile anachokiona kuwa cha kuudhi. Katika hali fulani, unyanyasaji unaweza kuwa kosa la jinai na unaweza kusababisha amri ya kuzuliwa au kufunguliwa mashtaka.

Unyanyasaji unaweza kuwa wa aina mbalimbali, na inayojulikana zaidi ni:

- maoni ya kuashiria ngono
- matusi/vichekesho vya kibaguzi
- maneno ya kudhalilisha
- kujipendekeza kusikotakiwa

Unyanyasaji unaweza kuwa wa makusudi, usiokusudiwa na wa kulazimishwa.

Unyanyasaji unaweza kuwa wa moja kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kwa moja katika mwenendo ambao mtu huyo anajua au anafaa kujua:

- husababisha madhara au kuchochea desturi kwamba madhara yanaweza kufanywa kwa mwathiriwa au mtu wa karibu bila sababu:



- kufuata, kutazama, kufuatilia au kumdhumu mwathiriwa au mtu anayehusiana naye, au kuzurura nje ya au karibu na jengo au mahali ambapo mwathirika au jamaa wa karibu, anafanya kazi, anafanya biashara au masomo.
- kujihusisha na mawasiliano ya maongezi, kielektroniki au mengine yoyote yanayomlenga mhasiriwa au jamaa wa karibu, kwa njia yoyote ile, iwe mazungumzo yanaendelea au la.
- kutuma, kuwasilisha au kusababisha uwasilishaji wa barua, telegramu, vifurushi, faksi, barua pepe au vitu vingine kwa mlalamishi au mtu anayehusiana au kuviacha pale vitapatikana, kupewa au kuletwa kwa mlalamishi au jamaa wa karibu.

- husababisha unyanyasaji wa kijinsia kwa mwathiriwa au mtu anayehusiana.

Uonevu na Unyanyasaji wa Mtandao

Uonevu unaweza kutokea mahali popote, nyumbani, shuleni, uwanja wa michezo, maeneo mengine katika jamii na mtandaoni (unyanyasaji wa mtandaoni). Uonevu kwa kawaida hufanyika kwa muda mrefu na unaweza kusababisha madhara ya kimwili na kihisia.

Athari za uonevu kwa watoto na watu wazima walio katika mazingira hatari mara nyingi hupuuza na zinaweza kusababisha dhiki kubwa, ambayo inaweza kuathiri afya au ukuaji wa mtu.

Maonevu ni kama vile:

- **Kimwili:** kusukuma, kugonga, kupiga,

- kufinya na aina nyingine za ukatili au vitisho.
- Kihisia:** kubagua, kutesa, kudhihaki kudhalilisha.
- Rangi:** dhahaka za rangi, michoro, ishara.
- Kingono:** mgusano wa kimwili usiofaa dhahaka za ushoga, maoni ya matusi

Uonevu unaweza kutokea kati ya:

- Mtu mzima na kijana.
- Kijana na kijana mwingine.
- Mzazi na mtoto wake

Kwa kuwa mchezo una ushindani wa kawaida, fursa ya uonevu inaweza kuongezeka. Mifano ni kama vile:

- Mshiriki kudhihakiwa kwa sababu ya kuwa mshindani dhaifu.
- Wazazi wakimsukuma mtoto wao kwa bidii kushiriki na / au kuongeza utendaji wake.
 - Mwezeshaji akichukua mtazamo wa kushinda kwa lazima.
 - Viongozi au wazazi/walezi wakiweka shinikizo isiyostahili kwa washiriki ili kupata matokeo.

Unyanyasaji wa Marika

Unyanyasaji kati ya rika ni “unyanyasaji wa kimwili, kingono, kihisia na kifedha na udhibiti wenye shuruti unaofanywa katika uhusiano wa mtoto au kijana, ikijumuisha mahusiano ya karibu, urafiki na ushirikiano wowote wa rika”.

Mifano ni kama vile:

- Kulazimishwa kushiriki katika vitendo vya ngono.

- Vitisho vya kudungwa kisu kwenye vyumba vya kubadilishia nguo au vyoo.
- Kupigwa picha za ngono bila idhini.
- Ubakaji wa vijana shuleni/chuoni, kwenye karamu na ugenini wakati wa safari.
- Kutengwa na vikundi vya kijamii kwa sababu ya kabila au lugha wanazozungumza au kutozungumza.
- Kueneza uvumi na kusambaza fitina kuwahu.

Dhuluma za Kinyumbani – Inajumuisha Ukatili kati ya Wapenzi wa Karibu (IPV) au Mtoto Kushuhudia wapenzi wakinyanyasana

Dhuluma za kinyumbani, pia huitwa “ukatili majumbani” au “ukatili kati ya wapenzi wa karibu (IPV)”, zinaweza kufafanuliwa kuwa mtindo wa

tabia katika uhusiano wowote unaotumiwa kupata au kudumisha mamlaka na udhibiti dhidi ya mpenzi.

Dhuluma za kinyumbani kwa kawaida hudhihirika kama mtindo wa dhuluma dhidi ya mpenzi katika uchumba au uhusiano wa kifamilia, ambapo mnyanyasaji huwa na nguvu na udhibiti juu ya mwathiriwa.

Waathiriwa wa dhuluma ya kinyumbani wanaweza pia kuwa watoto walioshuhudia unyanyasaji kati ya wapenzi wa karibu nyumbani, au mwanafamilia mwingine yeyote.

Dhuluma ya kinyumbani inaweza kutokea kwa mtu yeyote wa rangi, umri, mwelekeo wa kijinsia, dini, jinsia, hali ya kijamii na kiuchumi au kiwango chochote cha elimu. Matukio haya hayana tofauti na kwa kawaida huongezeka mara kwa mara kwa kutegemea na hali. Dhuluma ya kinyumbani inaweza kusababisha majeraha mabaya ya kimwili au kifo.



Unyanyasaji wa Kifedha

Unyanyasaji wa Kifedha unahusu matumizi mabaya ya rasilimali za kifedha au matumizi mabaya ya udhibiti wa kifedha katika uhusiano ambao unategemea kuwepo kwa uaminifu. Watu wazima walio katika hatari, wanawake walio katika mahusiano mabaya na wazee wanaweza kuwa katika hatari ya kunyanyaswa kifedha. Kwa mfano, kumekuwapo na matukio ya wazazi kutapeliwa fedha kwa ahadi ya mtoto wao kupewa nafasi za kushiriki majaribio katika vilabu vya kulipwa kisha ikabainika kwamba majaribio hayo hayapo.

Kupumbaza

Urafiki wa kupumbaza unaweza kufanywa na wanaume na wanawake na unaweza kutokea mtandaoni ama watu kukutana moja kwa moja. Inaweza kufanywa na mtu ambaye mtoto au kijana anamjua au na mgeni.

Urariki wa kupumbaza ni pale mtu anafanya kila awezalo ili kujenga uhusiano wa kihisia na mtoto kwa lengo la kuaminika kwa madhumuni mahususi ya unyanyasaji wa kingono au ukandamizaji.

Washiriki wengi hawataelewa kuwa wameandaliwa na kwamba watanyanyaswa baadaye. Wanaweza kuwa na hisia tata, kama hisia ya uaminifu, kutamaniwa au kupendwa, pamoja na hofu, dhiki na kuchanganyikiwa. Wanyanyasaji wanaweza kutumia muda mwingi na juhudi ili kuaminiwa na watoto, na ikiwezekana kuaminiwa na familia zao kupitia:

- kutoa ushauri na uelewa.
- kununua zawadi, kama vile vifaa.

- kuwasikiza watoto wakijieleza.
- kwa kutumia vyeo au sifa zao za kitaaluma.
- kuwapeleka katika ziara, matembezi au likizo.

Punde tu wanapoanza kuaminiwa, waandaji watatumia vibaya uhusiano huo kwa kumtenga mtoto na marafiki au familia na kumfanya mtoto ahisi kumtegemea mnyanyasaji huyo pekee. Watatumia njia yoyote ya mamlaka au udhibiti kumfanya mtoto amini kuwa hana chaguo ila kufanya yale wanayotaka. Wanyanyasaji wanaweza kuanzisha ‘siri’ ili kudhibiti au kumtisha mtoto. Wakati mwingine watandanganya mtoto au kumfanya aone aibu au hatia kuwazuia kumwambia mtu yeyote kuhusu unyanyasaji huo.

Mtoto au mtu mzima anapoandaliwa mtandaoni, waandaji wanaweza kujificha wasijulikane wao ni nani kwa kutuma picha au video za watu wengine. Wakati mwingine picha ni za mtu mdogo kuliko mwandaaji ili kujaribu kupata uaminifu wa “kirika”. Wanaweza kulenga mtoto mmoja mtandaoni au badala yake wawasiliane na watoto wengi kwa mfululizo wa haraka na kusubiri wawajibaji.

Itikadi Kali

Itikadi kali inahusu sherehe za jandoni, ikiwa ni pamoja na matambiko, mashindano na shughuli nyingine, zinazohusisha unyanyasaji, kudhulumu au udhalilishaji kama njia ya kuingiza mtu katika kikundi, kama vile timu ya michezo. Itikadi kali mara nyingi hutokea pale ambapo kuna ukosefu wa usimamizi wa watu wazima. Mara nyingi hutokea pamoja na

matumizi ya pombe na kuhusisha shughuli za ngono zisizohitajika. Itikadi kali mara nyingi hupendelewa kimakosa na shirika la michezo kama sehemu ya utamaduni wake.

Ulanguzi wa binadamu

Ulanguzi wa binadamu ni mchakato wa kuajiri, kuhamisha au kusafirisha watoto au watu wazima ili kuwakandamiza, iwe kwa kazi ya kulazimishwa au kuwauza. Mara nyingi wao hupelekwa mbali na nyumbani kwao na kulazimishwa kufanya kazi katika biashara ya ngono. Kumekuwapo na visa vya ulanguzi wa binadamu unaohusishwa na michezo barani Afrika ambapo watoto wamekuwa wakisafirishwa hadi kwenye kambi ghushi za mafunzo ya michezo na kisha kunyanyaswa, kutelekezwa na kukandamizwa.

Ni nani anayedhulumu?

Pengine umesikia neno “hatari isiyojulikana” na labda umeona wazazi wakiwapa watoto wao ushauri kuhusu hatua za kuchukua iwapo watakutana na mtu wasiyemjua.

Mbali na watu wa familia ni watu gani wengine ambao watoto wanaweza kuwaamini kisha wakawa katika hatari ya kudhulumiwa? Mtu anayeshikilia nafasi ya kuaminika, ambapo mtu yuko katika nafasi ya mamlaka juu ya mtu mwingine. Mifano ni kama vile:

- Mwalimu
- Kiongozi wa dini
- Daktari
- Kocha wa michezo
- Kijana
- Rafiki (mwanarika)
- Afisa wa polisi

Walimu wa shule, mapadri, madaktari na makocha wa michezo, pamoja na wengine wakiwamo wanafamilia na wanarika, hukamatwa na kuhukumiwa kila mwaka kwa kuwadhulumu watoto.

Watu walio katika vyeo vya kuaminiwa wanaweza kutumia vibaya nafasi hizo kuwanyanya watoto. Hali ni sawa pia kwa watu wazima walio katika mazingira hatari. Kuaminiana kati ya pande hizo mbili ndiko kunakomwezesha mhusika kuwa karibu sana kwa waathiriwa ili kuwanyanya. Tunajua kwamba mtu yeyote anaweza kumdhuru mtoto.

Unyanyasaji na dhuluma mara nyingi hutokana na matumizi mabaya ya mamlaka, yaani matumizi yasiyofaa ya nafasi ya ushawishi, uongozi au mamlaka ya mtu dhidi ya mwingine. Watoto wengi na watu wazima ambao wamedhulimiwa kingono walinyanyaswa na watu waliowafahamu.

Utendakazi Duni

Tunapozungumza kuhusu utendakazi, tunarejelea jinsi tunavyotenda wakati wa kutekeleza majukumu yetu katika mazingira mbalimbali ya michezo. Kwa mfano, jinsi tunavyofundisha spoti/ Michezo kwa Maendeleo kwa watoto au watu wazima walio katika mazingira hatari.

Utendakazi duni unarejelea tabia ya mtu binafsi aliye na jukumu kazini isiyikidhi vigezo vinavyohitajika katika shirika (kwa kawaida hivi huangaziwa katika Kanuni ya Maadili kwenye shirika).

Wale wanaofanya kazi na watoto pamoja na watu wazima walio katika mazingira hatari katika michezo wanapaswa kwanza kufanya kazi kulingana na kanuni ya "Kutodhuru". Wanafaa kuhakikisha kwamba mwenendo wao unalinda watoto au watu wazima walio katika mazingira hatari wanaokutana nao katika michezo. Wanapaswa kuonyesha desturi bora kila wakati na kufanya kazi ili kuandaa mipango salama, jumuiishi na ya kufurahisha kwa watoto na watu wazima kushiriki katika michezo.

Utendakazi duni unaweza kukosa kuwa na hatari ya moja kwa moja au kudhuru kimakusudi watoto au watu wazima walio katika mazingira hatari, lakini unaweza kuleta mazingira yenye uwezekano mkubwa wa unyanyasaji, dhuluma au ukandamizaji.

Athari za unyanyasaji kwa mtoto au mtu mzima zinaweza kuwa kubwa na kusababisha mtoto au mtu mzima kuhisi kutokuwa na furaha, kukandamizwa au kutothaminiwa. Unyanyasaji mara nyingi ni aina ya dhuluma inayoendelea kusababisha dhiki kutegemea na kuendelea au kurudiwa kwake, ambako kwa kawaida huwa ni kwa maneno.

Dhuluma, iwe ya muda mfupi au ya muda mrefu, inaweza kuwa mbaya sana kwa mtoto au mtu mzima na athari ya unyanyasaji mara nyingi hudumu maisha yote.

Utendakazi duni unanaweza kumdhuru mtendaji (mwezesaji au cheo kingine katika mchezo) na shirika (klabu au mradi), na pia kwa watoto au watu wazima wanaokumbana nao. Mifano ya utendakazi duni ni pamoja na, lakini si tu, kufunza au kufundisha ukiwa unakuka pombe, kuvuta sigara wakati wa kikao, kutumia lugha ya matusi mbele ya au kuwaelekea washiriki, au kutokuwa mwangalifu au kuwajali washiriki. Utendakazi duni unaweza kuleta mashtaka ya kutelekeza baada ya kushindwa kuwa mwangalifu au kutojali kisha kusababisha ajali.

Utendakazi duni wakati mwingine unaweza kusababisha au kuchochea mazingira ya unyanyasaji au dhuluma. Unaweza pia kuleta wasiwasi kuhusu malengo ya mtendaji, hata pale ambapo hakuna madhara anayokusudia. Kwa mfano, ikiwa mwezesaji anamjali mtoto mmoja kupita kiasi, anasafirisha watoto mara kwa mara kwenye gari lake au kupendelea kugusuna kimwili na watoto kinyume na kawaida, inaweza kuibua wasiwasi.

Kanuni za maadili na miongozo bora ya utendakazi hutumika katika michezo ili kuondoa tabia mbaya na kusaidia kuwalinda washiriki kwa kushughulikia na kuzuia mapema dhuluma mbalimbali.

MASHIRIKA

Mashirika yote, taasisi, mashirikisho, shule na vilabu vinavyofanya kazi katika spoti na Michezo kwa Maendeleo, viwe vidogo au vikubwa, vinapaswa kuwa na sera na hatua zitakazohakikisha watoto, vijana na watu wazima walio katika mazingira hatari wanaweza kushiriki katika michezo na shughuli nyingine katika mazingira salama, jumuishi na ya kufurahisha. Yafuatayo ni baadhi ya mambo ambayo shirika linapaswa kufanya:

- Kutumia sera ya ulinzi.
- Kuanzisha utamaduni wa ulinzi katika shirika.
- Jenga mazoea ya kuwasikiliza washiriki – watoto, vijana na watu wazima.
- Chagua maafisa wa kuongoza ulinzi.
- Tengeneza kanuni za maadili.
- Anzisha mchakato salama wa kuwaajiri wafanyakazi wote na watu wa kujitolea.
- Hakikisha wafanyakazi wote na wanaojitolea wana mafunzo ya msingi ya ulinzi.
- Anzisha rasmi mfumo wa kuripoti matatizo.
- Anzisha uhusiano na watu muhimu katika idara ya polisi na wizara ya huduma kwa jamii.
- Fanya uchunguzi kuhusu hali hatarishi mara kwa mara na kutekeleza mpango wa ulinzi.
- Wajulishe washiriki, wazazi/walezi na jamii kwa jumla mipango iliyopo kwa ajili ya ulinzi.

- Hakikisha mashirika ya washiriki wanazingatia sera ya ulinzi.
- Fuatilia sera ya ulinzi na mikakati kisha uikague mara kwa mara.

Kuandaa Sera

Mashirika yote, bila kujali ukubwa, ambayo yanatekeleza shughuli za spoti au Michezo kwa Maendeleo kwa watoto au watu wazima walio katika mazingira hatari yanapaswa kuwa na ulinzi katika sera ya michezo. Kwa vile maslahi ya mtoto yana umuhimu mkubwa, kila shirika linapaswa kuwa na vigezo vya chini kabisa vya sera ya ulinzi wa mtoto lakini yakumbuke kuwa njia bora ni kulinda kila mtu anayeshiriki au anaathiriwa na shughuli za shirika. Mashirika mengine yana sera na hatua tofauti za kuwalinda watoto na watu wazima walio katika mazingira hatari.

Sera ya ulinzi ni taarifa ya kusudi inayoonesha kujitolea katika kuwalinda watoto wanaohusika katika michezo dhidi ya madhara ya aina yoyote za hutoa mfumo ambamo taratibu zinatengenezwa.

Sera ya ulinzi inatoa maelezo ya wazi kwa kila mtu kuhusu kinachohitajika katika ulinzi wa watoto na watu wazima walio katika mazingira hatari. Inasaidia kuunda mazingira salama na bora kwa washiriki na kuonesha kwamba shirika limechukulia kwa uzito jukumu la utunzaji. Pia inazingatia mambo mahususi ambayo yanaweza kuwaacha baadhi ya watoto na watu wazima kuwa hatarini zaidi.

Sera za ulinzi zinapaswa kuidhinishwa na usimamizi wa shirika pamoja na wafanyakazi wakuu na zitumike kujenga utamaduni wa ulinzi ndani ya shirika.

Sera nzuri inafaa kuwa:

- iliyoandikwa kwa uwazi na rahisi kuelewa.
- kueleza jinsi shirika linavyoelewa na ufafanuzi wa aina zote za madhara.
- ieleze wazi msimamo wa shirika katika kuwalinda watoto na watu wazima walio katika mazingira hatari kwenye nyanja zote za kazi zao.
- iwe wazi kuhusu ni nani anayehusika na sera hiyo.
- iwe wazi kwamba watoto wote na watu wazima walio katika mazingira hatari wana haki sawa za kulindwa.
- kupitishwa na usimamizi pamoja na wafanyakazi wakuu katika shirika.
- iwe wazi kwamba utekelezaji wa sera ipo chini ya wasimamizi na wafanyakazi wakuu.
- imesainiwa na wafanyakazi wote, wakiwemo wa kujitolea, washiriki, wazazi/walezi na washirika wa huduma za mradi.
- imeandaliwa na kukaguliwa mara kwa mara kwa kushauriana na washiriki wa mradi, wakiwamo watoto, wazazi/walezi na wafanyakazi.
- inayoambatana na hatua za kutekeleza sera ili iwe zaidi ya tamko la kujitolea.

Wakati wa kuunda sera ya ulinzi, sheria ya kitaifa na mifumo ya ulinzi nchini inapaswa kuzingatiwa. Kunaweza kuwa na mahitaji maalumu yaliyowekwa katika sheria ya kitaifa kuhusu watu wanaofanya kazi na watoto au watu wazima walio katika mazingira hatari, kama vile hitaji la kupata kibali cha polisi ambacho kinaonesha kwamba mtu hajatenda kosa ambalo lingemzuia kufanya kazi na watoto au watu wazima wenye matatizo ya kiakili. Ufahamu kuhusu mahitaji ya lazima ya kuripoti na ni nani anayeweza kupokea ripoti pia lazima izingatiwe.

Mahitaji ya ulinzi yaliyowekwa na mashirika ya wazazi kama vile mashirikisho ya michezo ambayo yanaweza kuwa washirika au sera za kitaifa wa kulinda michezo pis yanapaswa kutiliwa maanani.

Yaliyomo katika Sera ya Kulinda yanaweza kujumuisha vipengele vifuatavyo:

UTANGULIZI – ikiwa ni pamoja na kurejelea Azimio la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu na/au, mahususi kwa ajili ya watoto, Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Mtoto.

USULI – Unatoa muhtasari wa hitaji la kuwalinda watoto na watu wazima walio katika mazingira hatari kwenye mazingira mbalimbali ya Michezo kwa Maendeleo.

FASILI – aina tofauti za madhara kwa watoto au watu wazima walio katika mazingira hatari ambayo wanaweza kukabiliwa nayo, kama vile kunyanaswa, kudhulumiwa, kutelekezwa na kukandamizwa.

LENGO – inaweka madhumuni ya sera ili kuwalinda watoto, watoto na watu wazima walio katika mazingira hatari, au washiriki wote.

KIWANGO CHA UTENDAJI – hii ni muhimu ili kuhakikisha kwamba wote wafanyakazi, watu wa kujitolea, washiriki, wazazi/walezi na washirika wanazingatia kiwango cha utendaji wa sera.

KAZI NA MAJUKUMU – kwa masharti ya utekelezaji wa sera, zinazotumika kwa washiriki wote na yale ambayo yamepewa bodi ya usimamizi na wafanyakazi maalum.

KANUNI YA MAADILI – kuweka viwango vinavyokubalika kwa mienendo katika shirika. Kanuni za maadili zinalenga kukuza utendaji bora.

UFUATILIAJI NA UHAKIKI – jinsi utekelezaji wa sera utafuatiliwa, kama vile kuripoti mara kwa mara kwa bodi ya usimamizi na ni mara ngapi itakaguliwa, kama vile kila mwaka.

TARATIBU ZA KURIPOTI – jinsi matukio yanafaa kuripotiwa kwa lazima kwa kuzingatia mahitaji ya mwongozo wa kuripoti na hatua za ndani za kuripoti.

TARATIBU ZA KUSHUGHULIKIA MATUKIO – jinsi maamuzi hufanywa kwa kuwasilisha masuala kwa mamlaka au kufanya uchunguzi wa ndani,

taratibu za kinidhamu au rufaa, au tathmini ya utendakazi.

MASHARTI YA MUDA – ambayo yameangazia mamlaka ya kusimamisha watu binafsi kusubiri matokeo ya kesi za uhalifu au uchunguzi wa ndani, taratibu za kinidhamu au rufaa, au tathmini ya utendakazi.

KUFICHUA MAOVU – kushughulikia ulinzi wa watu wanaoripoti matatizo na adhabu kwa malalamishi ya kuudhi.

USIRI – unahitajika ili kuhakikisha kuwa ni wahusika pekee ndio ambao wanajua kuhusu tukio la madhara ili kumlinda mtoto au mtu mzima aliyekatika mazingira hatari.

TAARIFA YA KUJITOLEA (kwa kusaini)

Hatua na mifumo ya kutekelezwa, kama vile kuripoti na kushughulikia kesi, kunaweza kujumuishwa katika hati ya sera ya mashirika au kutayarishwa kuwa hati za kujitegemea.

Nguzo Kuu za Ulinzi

Nguzo Kuu za Ulinzi ni wafanyakazi au watu wa kujitolea ambao wamepewa jukumu la kuratibu utekelezaji wa Sera ya Ulinzi katika vitengo maalumu. Mtu au watu wanaweza kuteuliwa kushughulikia masuala yote ya ulinzi katika shirika na wengine wanaweza kuteuliwa kushughulikia masuala ya ulinzi katika maeneo tofauti ya mafunzo, kwa matukio au kambi za mafunzo na safari za mbali na nyumbani.

Wafanyakazi au watu wa kujitolea waliopewa jukumu la ulinzi wanaweza kujulikana kama maafisa wa ustawi au ulinzi.

Kulinda nguzo kuu ni pamoja na:

- kukuza desturi ya ulinzi katika shirika ili kuhakikisha mazingira salama na bora kwa washiriki wote.
- kuhakikisha kuwa shirika linatimiza wajibu wake wa kuwalinda watoto na watu wazima walio katika mazingira hatari.
- kuongoza tathmini za hatari na utekelezaji wa mipango ya ulinzi.
- kufanya kazi ya kuwa sehemu ya kwanza ya mawasiliano kwa watu

kuwasilisha matatizo kuhusu ustawi wa mshiriki au pale ambapo kuna madai ya unyanyasaji, dhuluma, kutelekezwa, ukandamizaji au utendakazi duni.

- kuanzisha mawasiliano na polisi pamoja na maafisa wa huduma za kijamii.
- kutunza kumbukumbu za matatizo yaliyoripotiwa na matokeo ya hatua zilizochukuliwa.
- kuwasilisha sera, mikakati ya ulinzi na kanuni za maadili kwa washiriki, wafanyakazi, watu wa kujitolea, wazazi/walezi na washirika.
- kuripoti masuala ya ulinzi kwa wasimamizi wakuu wa shirika.
- kuhakikisha wawezeshaji wanaokutana

mara kwa mara na watoto au watu wazima walio katika mazingira hatari wanakaguliwa ipasavyo na wanapata mafunzo ya ulinzimara kwa mara.

- kuhakikisha usiri ufaao unadumishwa.

Jinsi ya kuimarisha nguzo kuu za ulinzi pia kunafaa kufanywa kipaumbele – kama vile kuunda kikundi cha ushauri ili kuwasaidia katika kazi zote za ulinzi, kutoa usaidizi wa kuunda sera na taratibu za shirika, au kuruhusu fursa ya kujadili kesi kwa siri – bila kuachwa kujifanyia maamuzi magumu peke yao.

Kanuni za Maadili

Kanuni za maadili hufanua kiwango cha mienendo inayokubalika katika shirika na hulenga kukuza utendaji bora.



Mienendo ya Kihalifu

Mifumo ya Kushughulikia Haki
Kupitia Polisi



Mwenendo Usiokubalika

Kikao cha Ndani cha Masuala ya
Nidhamu



Utendakazi Duni

Ukaguzi wa Ndani wa Utendakazi

Pale ambapo wasiwasi unaibuliwa kuhusu tabia ya mwezesaji au mshiriki katika shirika au kuhusu mtu mwingine nje ya shirika, tabia inayodaiwa inaweza kuwa:

- **Mhalifu** – madai ya ukiukaji wa sheria inayohitaji kesi kuripotiwa kwa polisi na inaweza kusababisha mashtaka na baadaye kupitishwa katika taratibu za kushughulikia kesi.
- **Isiyokubalika** - madai ya ukiukaji wa kanuni za maadili ambayo yanachukuliwa kuwa jambo zito na linaweza kuhitaji uchunguzi wa ndani na hata kutoa adhabu ya kinidhamu/rufaa kusikilizwa
- **Utendakazi duni** – madai madogo ya ukiukaji wa kanuni za maadili ambayo yanaweza kuhitaji kushughulikiwa, kama vile tathmini ya utendaji.

Mashirika yanapaswa kujitahidi kuondoa utendakazi duni ambao, ingawa unaweza kukosa madhara ya moja kwa moja au kudhuru kwa makusudi, wakati mwingine unaweza kusababisha mazingira ambayo yanashindwa kukabili unyanyasaji, dhuluma, kutelekezwa au ukandamizaji.

Mashirika yote ya Spoti na Michezo kwa Maendeleo yanapaswa kuwa na kanuni za mtagusano kwa watu wote wa kujitolea na wafanyakazi, kanuni hizo huweka viwango vya maadili vinavyolenga kuwalinda wale wanaoshiriki katika shughuli za shirika. Watumishi wote wa kujitolea na wafanyakazi wanapaswa kuheshimu Kanuni za Maadili.

Wakati wa kuandika kanuni tofauti za maadili kwa vikundi tofauti, yafuatayo yanafaa kuzingatiwa:

- kujumuisha taarifa kuhusu maadili katika michezo, kwa mfano, kuwashughulikia watu kwa utu, heshima, usikivu na haki.
- kubainisha mwongozo na matarajio kuhusu shughuli ambazo ni pamoja na muda uliotumika mbali na nyumbani, ikiwa ni pamoja na kuwaweka watoto kwenye uangalizi wa wengine na kukaa usiku kucha.
- mwongozowa jinsi ya kufanya kazi na watoto ambao wana ulemavu au mahitaji maalum.
- mwongozo kuhusu njia bora za kudhibiti mienendo ya watoto ambayo haihusishi adhabu ya kimwili au aina nyingine yoyote ya udhalilishaji au ukandamizaji na inahusu uwezo, umri na jinsia.

- mwongozo wa mienendo inayotarajiwa na inayokubalika ya watoto kwa wengine, hasa watoto wengine.
- matokeo ya wazi ya kutofuata miongozo ya mienendo ambayo inahusishwa na taratibu za kinidhamu za shirika.

Wakati wa kuunda kanuni za maadili katika viwango tofauti vya shirika lako, ni desturi nzuri kushauriana na washiriki, wakiwamo watoto, wazazi/walezi, wafanyakazi na watu wa kujitolea.

Mfano wa Kanuni za Maadili kwa Wawezeshaji wa S4D

Ninaahidi kujitolea kwa uthibitisho wangu kuwa Mwezeshaji wa (S4D) kwa kufuata Kanuni ya Maadili ya (S4D).

Ninaelewa na kuheshimu wajibu wa nafasi yangu kama mfano wa kuigwa kwa washiriki wote, hasa watoto na watu wazima walio katika mazingira hatari.

Nitadumisha utendakazi bora na:

- kuhakikisha vipindi vya Michezo na S4D ni vya kufurahisha, salama na jumuishi.
- kuheshimu haki, utu na thamani ya kila mshiriki bila kubagua kwa sababu ya umri, rangi, rangi ya ngozi, kabila, taifa, au asili ya kijamii, jinsia, ulemavu, lugha, dini, maoni ya kisiasa au maoni yoyote, utajiri, kuzaliwa au hali yoyote nyingine, mwelekeo wa kijinsia au sababu nyingine yoyote.
- kuripoti kila mara tatizo lolote kuhusu utendakazi duni au unyanyasaji kwa afisa wa ulinzi aliyeteuliwa. ninakubali kwamba lazima niripoti tatizo lolote ambalo ninaweza kuwa nalo – sina hiari ya kutochukua hatua.
- kuongoza kwa mfano katika suala la uchezaji bora na kuwa kielelezo kwa wengine, wakiwamo watoto – hii ni pamoja na kutokunywa pombe, kutumia dawa za kulevyu au kutumia lugha chafu, ya kibaguzi, chuki kwa wapenzi wa jinsia moja au lugha nyingine za kibaguzi mbele ya watoto au watu wengine.
- kuheshimu nafasi yangu inayoaminiwa na kudumisha mipaka ifaayo na watoto, vijana na watu wazima walio katika mazingira hatari.
- kufanya kazi katika mazingira ya wazi na kuepuka kukaa pekee yangu na watoto, vijana au watu wazima walio katika mazingira hatari mbali na watu wengine.
- kufika kwa muda wa kutosha ili kuanzisha shughuli na kuhakikisha kuwa tathmini za hatari zinafanywa kwa shughuli, miradi na matukio yote yanayowahusisha watoto, vijana na watu wazima walio katika mazingira hatari.
- kuhakikisha watoto, vijana na watu wazima walio katika mazingira hatari wako salama kwa kuwasimamia ipasavyo na kutumia mbinu salama za mafunzo na ujuzi.
- kupinga aina yoyote ya tabia ya uonevu miongoni mwa watoto, vijana au watu wazima walio katika mazingira hatari.
- kuwasiliana kwa njia inayofaa, inayozingatia umri na watoto, kuhakikisha kwamba hawaaibiki kamwe.
- kutoa fursa muhimu za kuwawezesha watoto na vijana kushiriki katika mchakato wa kufanya maamuzi.
- kuhakikisha taarifa za siri hazitolewi isipokuwa kwa idhini ya wazi ya wale wote wanaohusika au kesi inapotaka kufichuliwa kwa mamlaka husika.
- kuhimiza washiriki wote kuwajibika kwa mwenendo na utendaji wao wenyewe ndani na nje ya uwanja wa michezo.
- kuwasiliana kwa uwazi na washiriki wote, au wazazi/walezi inapobidi, nikiweka wazi matarajio yangu kwao na kile wanachoweza kutarajia kutoka kwangu.

Sitawahi:

- kushiriki au kuruhusu michezo yoyote inayochochea hali mbaya kwa maneno, kimwili au ngono, au kugusana kusikofaa kwa watoto, vijana au watu wazima walio katika mazingira hatari (kuepuka kugusa makalio, sehemu nyeti na matiti).
- kushiriki katika uhusiano wowote wa kimapenzi na mshiriki yeyote aliye chini ya umri wa miaka 18, ikiwa ni pamoja na kutoa maoni yanayochochea ngono kwa mtoto.
- kumwanda au kumkandamiza mtoto, kijana au mtu mzima aliye katika mazingira hatari kwa manufaa ya kibinafsi na ya kifedha.
- kushiriki katika matumizi mabaya ya mitandao ya kijamii – hii ni pamoja na kuwashirikisha watoto katika mazungumzo ya siri ya mitandao ya kijamii na kutowahi kutuma maoni ambayo yanaweza kuhatarisha ukuaji wao au kuwadhuru.
- kumfanya mtoto au mtu mzima aliye hatarini kulia au kumtisha au kumdhalilisha kama njia ya kumdhibiti.
- kujihusisha na tabia ya uonevu.
- kuruhusu ukiukaji wa sheria, aina yoyote ya dhuluma au matumizi ya vitu vilivyopigwa marufuku.
- kuumiza kimwili kwa makusudi au kutishia kuumumiza mtoto, kijana au mtu mzima aliye katika mazingira hatari – kugonga na kupiga ngumi kunaweza kuwa vitendo vinavyodhibitiwa katika baadhi ya michezo (ya mapigano) lakini kusiwe na nafasi katika michezo mingi.

DOWNLOAD 

[https://www.sport-for-development.com/imglb/downloads/safeguarding/giz-2021-en-sample-code-of-conduct-for-\(s4d\)-facilitators-safeguarding-in-sport-and-s4d-contexts.docx](https://www.sport-for-development.com/imglb/downloads/safeguarding/giz-2021-en-sample-code-of-conduct-for-(s4d)-facilitators-safeguarding-in-sport-and-s4d-contexts.docx)

Mchujo wa Wawezeshaji

Shirika lolote la Spoti au Michezo kwa Maendeleo linapaswa kuchukua hatua zote zinazofaa wakati wa mchakato wa kuajiri ili kuwazuia watu wasiofaa kufanya kazi na watoto, vijana au watu wazima walio hatarini.



Huenda kukawa na mahitaji ya kisheria katika nchi ambayo yanahitaji watu wanaofanya kazi na watoto, vijana au watu wazima walio katika mazingira hatari wakaguliwe ili kubaini rekodi ya uhalifu, au kuchunguzwa mara kwa mara dhidi ya wakosaji wa ngono au rejista za ulinzi wa watoto.

Angalau, mashirika yanapaswa kuwataka wafanyakazi na watu wa kujitolea wanaofanya kazi na watoto au watu wazima walio katika mazingira hatari kutoa cheti cha sasa cha kibali cha polisi kabla ya ushiriki wao au wakati wa mchakato wa kuajiriwa. Hatua hii inafaa pia kuwahusu watu wa kimataifa wanaojitolea ambao wanapaswa kuhitajika kuwasilisha cheti cha kibali cha polisi cha kimataifa.



Iwapo haiwezekani kupata cheti cha kibali cha polisi, shirika linapaswa kuomba hati ya kiapo iliyosainiwa ili kuthibitisha wafanyakazi na watu wa kujitolea hawajawahi kukabiliwa na madai ya unyanyasaji wa watoto au kuhukumiwa kwa makosa ya ngono au ya ukatili na hawajawahi kukabiliwa na kesi za kinidhamu zinazohusiana na kuwadhuru watoto au watu wazima walio katika mazingira hatari au wasiostahili kufanya kazi na watoto au watu wazima walio katika mazingira hatari katika nchi yoyote.

Pamoja na kupata cheti cha sasa cha kibali cha polisi au hati ya kiapo, mashirika ya Spoti na Michezo kwa Maendeleo yanaweza pia kuchukua hatua zifuatazo ili kutathmini ufaafu wa mtu kufanya kazi na watoto au watu wazima walio katika mazingira hatari:

- Uliza mtu huyo atoe majina ya watu wawili ambao wanamjua, wasiliana nao na uwaulize kuhusu uwezo wa mtu huyo katika kufanya kazi na watoto na watu wazima walio katika mazingira hatari katika miktadha ya Spoti na Michezo kwa Maendeleo.
- Angalia sifa za mtu na uzoefu kulingana na jukumu la mwezeshaji katika shirika, ikiwa ni pamoja na kama anatarajiwa kufunza michezo ambayo ana tajriba ya kufundisha.
- Mhoji mtu huyo na utathmini mtazamo wake kuhusu ulinzi na uzoefu wake wa kufanya kazi na watoto, vijana, au watu wazima walio katika mazingira hatari.
- Wakati wa usaili mpe mhojiwa mazingira ya halisi kuhusu ulinzi na umuulize jinsi angeshughulikia hali hiyo.
- Muulize mtu huyo kama amewahi kukataliwa katika kazi iliyohusisha kukutana na watoto au watu wazima walio hatarini au kama kuna chochote ili shirika lijue hilo linaweza kuathiri uwezo wake katika kufanya kazi na watoto au watu wazima walio hatarini.

Mafunzo ya Ulinzi

Shirika lolote linalofanya shughuli za Spoti au michezo kwa maendeleo na miradi linapaswa kuhakikisha kuwa kila mtu ambaye anakutana mara kwa mara na watoto na watu wazima walio katika mazingira hatari anapata mafunzo ya ulinzi kila mwaka. Kufanya hivyo kunaweza kujumuisha mafunzo ya kimsingi ya ulinzi yanayotolewa kama sehemu ya utangulizi wa mfanyakazi au watu wa kujitolea au taarifa ya kila mwaka.

Mashirika kadhaa ya Kimataifa ya Michezo yanatoa mafunzo bila malipo kuhusu ulinzi mtandaoni na kuna mashirika yasiyo ya kiserikali ambayo yanaweza kutoa mafunzo kibinafsi au mtandaoni.

Kamati ya Kimataifa ya Olimpiki - Kuwalinda Wanariadha dhidi ya Unyanyasaji na Dhuluma - <https://www.olympic.org/athlete365/courses/safeguarding-athletes-from-harassment-and-abuse/>

Tume ya Maadili ya Michezo Ayalandi - Somo 1 la Mafunzo ya Ulinzi Mtandaoni - <https://www.sportireland.ie/ethics/safeguarding-1-online-refresher>

UEFA - Kozi za Mtandaoni za Ulinzi katika Kandanda - <https://uefa-safeguarding.eu/learning>

FIFA - Ulinzi wa Mtandaoni katika Kozi ya Michezo kwa Wanafunzi Huria - <https://safeguardinginsport.fifa.com/open-learners/>

Sport Australia - Cheza kwa Sheria - <https://pbtr.ausport.gov.au/auth/login/?returnUrl=%2Fq%2FPBTR-CP>

Chama cha Makocha Kanada - Mafunzo ya Mchezo Salama - <https://safesport.coach.ca/participants-training>

Mashirika yanapaswa pia kuweka desturi ya ulinzi kwa kujumuisha ulinzi kama mada jumlishi na kipengele cha ajenda katika mikutano yote ya wafanyakazi na watu wa kujitolea.




Hatua za Kushughulikia Matatizo

Mashirika ya Spoti na Michezo kwa Maendeleo yanapaswa kuwa na hatua za kuripoti masuala ya unyanyasaji, dhuluma, kutelekezwa, ukandamizaji na desturi mbaya. Kila mtu anayehusishwa na shirika anapaswa kujua jinsi ya kuripoti matatizo yanayomkubwa, na kunapaswa kuwa na mwongozo wazi wa hatua kwa hatua kuhusu hatua za kuchukua katika hali tofauti tofauti.

Wakati wa kuunda kanuni za kukabili matatizo ya ulinzi, yafuatayo yanafaa kuzingatiwa:

- Kuna taratibu zilizo wazi ambazo hutoa mwongozo wa hatua kwa hatua kuhusu hatua gani ya kuchukua ikiwa kuna matatizo kuhusu watoto au watu wazima walio hatarini au ukuaji, ndani na nje ya shirika.
- Kuna mtu aliyeteuliwa katika shirika mwenye jukumu la kuongoza ulinzi, uwe ni ulinzi wa nguzo kuu au afisa wa ustawi/mlinzi.
- Shirika lako hutoa habari kwa washiriki, wazazi/walezi, watu wa kujitolea, wafanyakazi na washirika kuhusu haki zao, ni nani wanaweza kumtafuta wakiwa na matatizo na jinsi wanavyoweza kuripoti matatizo yao.
- Taarifa zinapaswa kupatikana kwa washiriki, wazazi/walezi, wafanyakazi, watu wanaojitolea na washirika kuhusu kile kinachoweza kutokea baada ya kufichua, katika umbo na lugha inayoweza kuwa rahisi kueleweka kwa kila mtu.
- Kuna mipango iliyowekwa kutoa msaada kwa washiriki, wafanyakazi na watu wa kujitolea wakati na kufuatia tukio, madai au malalamishi.
- Mchakato wa kushughulikia malalamishi kwa njia ya haki na yenye uwazi inayojumuisha rufaa mamlaka husika, au uchunguzi wa ndani unapofaa, pamoja na nidhamu au vikao vya rufaa na tathmini ya michakato ya utendakazi.
- Matukio yote, madai na malalamiko yanarekodiwa, kufuatiliwa na kuhifadhiwa kwa usalama. Chati za mtiririko ni muhimu na ni rahisi kutumia wakati watu wanatakiwa kuwa na uwezo wa kujibu kwa haraka.

Mchoro wa 2: Mfano wa Picha ya Mtiririko wa Kushughulikia Tukio



Mchoro hapo juu unaonesha njia ambayo matatizo mbalimbali ya ulinzi yanaweza kuchukua mwelekeo tofauti. Pale ambapo kuna masuala ibuka kuhusu usalama wa watoto au watu walio katika mazingira hatari au pale inaposhukiwa uhalifu umetendeka suala hilo lazima lipelekwe kwa polisi au afisa wa huduma za kijamii.

Pale ambapo rufaa imetolewa kwa polisi au afisa wa huduma za kijamii, shirika la Spoti au la Michezo kwa Maendeleo linapaswa kumsimamisha kazi mtuhumiwa, bila ya kumuonea mtu, ili kusubiri matokeo ya kesi ya uhalifu. Shirika linaweza pia kumsimamisha mtu kazi akisubiri uchunguzi wa ndani kuhusu ukiukaji wa kanuni za maadili au desturi mbaya ambapo kumekuwa na madhara kwa mtoto au mtu mzima aliye katika mazingira hatari. Ni muhimu kwa mashirika kuwa na kanuni za muda zilizojumuishwa katika sera zao za ulinzi ili ziweze kutumika wasimamisha kazi wafanyakazi wakisubiri matokeo ya kesi za uhalifu au uchunguzi wa ndani, kinidhamu/ rufaa au tathmini ya utendakazi.

Ni muhimu kwa watoto na watu wazima walio katika mazingira hatari, wazazi/walezi wao na wengine katika shirika wajue wanaweza kujitokeza na kufichua matatizo yao kwa maafisa wa vituo vya ulinzi ambao wanawategemea kama watu wazima wanaoaminika katika shirika.

Watu wa kujitolea na wafanyakazi wote wanaofanya kazi katika shirika wanapaswa kujua jinsi ya kupokea ufichuzi au matatizo kutoka kwa wazazi au watoto na jinsi ya kuwasilisha kwenye kituo cha ulinzi. Kuna uwezekano mkubwa kwa mzazi au mtoto kuzungumza na mwezesaji mara ya kwanza, ambapo

wanaweza kuwa na uhusiano mzuri zaidi – kuliko kulazimika kutafuta kituo cha ulinzi. Wafanyakazi na watu wa kujitolea wanafaa pia kutambua ishara mbalimbali la unyanyasaji na tabia za watu wazima ambazo zinaweza kusababisha madhara.

Ni muhimu pia kwamba watu wanaofichua matatizo wasaidiwe na mashirika, hasa ikiwa ni kwa watoto au watu wazima walio katika mazingira hatari. Vilevile, ni muhimu kumsaidia mtu anayeshtakiwa kwa uhalifu au tabia isiyokubalika au desturi mbaya hadi matokeo ya kesi yakatapoamuliwa. Taarifa kuhusu kila kesi inapaswa kusambazwa kwa msingi wa hitaji la kujua tu ili kuhifadhi usiri na kulinda masilahi ya wahusika wote.

Kutathmini Hatari za ulinzi

Kanuni ambazo mashirika ya spoti na michezo kwa maendeleo hutumia ili kuwalinda watoto na watu wazima walio katika mazingira hatari, zinaweza kuimarishwa kwa kufanya tathmini za hatari mara kwa mara na kuandaa mpango wa utekelezaji wa ulinzi.

Katika Sura ya 4 ya nyenzo hii, tunaangazia jinsi wafanyakazi, watu wa kujitolea, washiriki, wazazi/walezi, na wanajamii wengine wanaweza kufanya kazi pamoja.

Tathmini ya hatari hufanywa kwa kuzingatia:

- Maeneo yenye shughuli hatari zaidi
- Mazingira hatari maalumu kwa washiriki wetu
- Wawezeshaji na utendakazi wao
- Sera za shirika na jamii
- Mitindo ya maisha na taratibu
- Mazingira ya maisha ya kijamii
- Afya, kuzuia ajali na matatizo ya kiusalama

Tathmini ya hatari husababisha kuweka mipango ya utekelezaji wa ulinzi ambapo hatari zinafanywa kipaumbele, na kutambua hatua za kuchukuliwa ili kupunguza hatari.

Mawasiliano

Ni hasara kwa shirika kuwa na sera imara za ulinzi na mikakati ikiwa ni watu wachache pekee wanafahamu sera hizo katika shirika hilo. Ni wajibu wa kila mtu kuwalinda watoto, vijana na watu wazima walio katika mazingira hatari na wanapaswa kuwa na taarifa kuhusu sera, kufahamishwa kanuni za maadili, kujua jinsi ya kuripoti matatizo na kushauriwa wakati wa tathmini ya sera.

Ikiwa shirika lina wavuti, maelezo kuhusu ulinzi na jinsi ya kuripoti matatizo yanapaswa kuwekwa kwenye wavuti na kufikiwa kwa urahisi kupitia kitufe au kiungo kwenye ukurasa wa wavuti huo..

Watoto na watu wazima walio katika mazingira hatari, wazazi/walezi, wafanyakazi, watu wa kujitolea na wanajamii wanapaswa kushauriwa kuhusu mahali pa kupata usaidizi na msaada. Tuna wajibu wa kuhakikisha ushauri na usaidizi unapatikana ili kusaidia watu wafanye kazi yao katika kulinda watoto na watu wazima walio katika mazingira hatari ili wajue ni nani wanaweza kumtafuta kwa ajili ya usaidizi.

Mashirika ya Spoti na Michezo kwa Maendeleo yanapaswa kuzingatia mbinu nyingine ambazo zinaweza kuwapa watoto na watu wazima walio katika mazingira hatari ushauri na usaidizi kuhusu jinsi ya kujilinda na kulinda wengine. Katika sura ya 4 tunaangazia ufundishaji wa stadi za maisha za kinga zinazolenga kuwasaidia washiriki katika shughuli za michezo kujiepusha na madhara kwa kutumia mbinu ya Michezo kwa Maendeleo.

Ushirikiano

Kuchukua hatua za haraka ili kuwalinda watoto na watu wazima walio katika mazingira hatari wakati malalamishi yameibuliwa ni vizuri kuwa na mahusiano na watu binafsi na mashirika ambayo yanaweza kukusaidia. Mashirika ya Spoti na Michezo kwa Maendeleo yanapaswa kubainisha watu wakuu ambao wanaweza kuwasiliana nao katika polisi na afisa wa huduma za kijamii katika eneo husika. Kwa kuanzisha uhusiano na watu wanaofaa, yanaweza kupata usaidizi na ushauri wa haraka tatizo linapotokea. Akiwa ni polisi, huyu anaweza kuwa afisa aliyepewa jukumu la kushughulikia masuala ya ulinzi wa watoto katika jamii. Huduma za kijamii zinaweza kutolewa na serikali, kupitia afisa wa huduma za kijamii anayetambuliwa au kupitia NGO inayojishughulisha na masuala ya ulinzi. Kumtambua mtu anayefaa ili kuzungumza na kushiriki naye sera



na mikakati kunaweza kusaidia sana anapotafuta usaidizi na ushauri.

Changamoto zinaweza kuibuka wakati washirika wawili au zaidi wanapohusika katika kuagiza, kufadhili na kutoa shughuli fulani. Hali zimetokea ambapo watoto wamewekwa hatarini au kujeruhiwa, kwa sababu ya kukosa ulinzi au kwa sababu washirika hawakufahamu majukumu yao husika. Kwa hiyo ni muhimu kwa kila mtu anayehusika katika mchakato huu kuwa na uhakika kwamba mikakati yote inayofaa imezingatiwa ili kuwalinda watoto wanaohusika.

Pamoja na mashirika yanayohusika kama vile wafadhili au mashirika mengine ya spoti na Michezo kwa Maendeleo, ni muhimu kushawishi na kukuza matumizi na utekelezaji wa mikakati za kulinda watoto na watu wazima walio hatarini. Mashirika yanafaa kushiriki mafunzo ya jinsi ya kufanya michezo kuwa salama kwa watoto na watu wazima walio hatarini. Sera ya ulinzi ya shirika lako inapaswa kuwa sehemu muhimu ya makubaliano yoyote ya ushirikiano. Ambapo mashirika yanahudhuria hafla unayoandaa, kama vile mashindano, unaweza kutaka kuwafanya wajisajili kwa sera yako ya ulinzi ili wafanyakazi wao, watu wa kujitolea na washiriki wajumuishwe katika utendaji wa sera yako wakati wa tukio.

Ufuatiliaji na Tathmini

Sera ya ulinzi wa shirika inahitaji kuwa hati ya moja kwa moja ambayo inaweza kubadilishwa kwa kujifunza na ambapo mikakati ya ulinzi inaweza kuboreshwa kila mara ili kupunguza hatari kwa watoto na watu wazima walio hatarini. Bodi ya usimamizi na wafanyakazi wakuu inapaswa kupokea taarifa za kila mara kuhusu ulinzi katika shirika, kisha kuwe na tathmini ya sera na desturi iliyopo kila mwaka.

Sera na mikakati ya ulinzi zinaweza pia kutathminiwa hasa kwenye sehemu ambazo kumekuwapo na mafunzo kutokana na kesi fulani, ambapo kuna mabadiliko ya sheria au pale kuna mabadiliko makubwa katika jinsi shirika linavyofanya kazi.

Tathmini zinafaa kuhusisha mashauriano na watoto na watu wazima walio hatarini, wazazi/walezi, wafanyakazi, watu wa kujitolea na wengine.

Uangalizi wa mara kwa mara katika ngazi ya kishirika unaweza pia kutambua mienendo na kusaidia shirika kushughulikia kwa haraka masuala yanayoibuka.

Mikakati inafaa kuwekwa ili kurekodi jinsi kesi inavyoendelea, na tathmini za hatari kufanywa mara kwa mara katika ngazi ya kishirika kuhusu matukio au shughuli maalum.

Ngazi ya juu katika shirika ina jukumu la kuongoza utekelezaji wa mchakato wa uangalizi na tathmini.

Kutoa taarifa kwa wanachama, wanajamii na wafadhili kuhusu ulinzi katika matatizo mbalimbali, na jinsi yalivyoshughulikiwa (au yalitatuhiwa), na kulinda usiri wa watu wanaohusika, ili kusaidia kujenga utamaduni wa uwajibikaji shirikishi kwa ajili ya ulinzi na utunzaji.

Covid-19 - Athari kwa Sera na Mikakati ya Ulinzi

Umuhimu wa kulinda sera na mikakati inayochukuliwa kuwa nakala ya maandishi yanayoweza kubadilishwa ambazo zinakaguliwa mara kwa mara, zinaonesha mafunzo tuliyojifunza na zinatumiwa kunapokuwa na mabadiliko makubwa katika muundo wa shirika au mikakati ilianguziwa mwaka 2020 wakati ulimwengu ulipokumbwa na Janga la Covid-19.

Janga hili limekuwa na athari kubwa kwenye shughuli za shirika la Spoti na Michezo kwa Maendeleo, huku watoto na vijana wakilazimika kujitenga na kunyimwa fursa ya kukutana kucheza na kukuza stadi za maisha katika mazingira salama, jumuishi na ya kufurahisha.

Punde tu shughuli za Spoti na Michezo kwa Maendeleo zilivyositishwa na masharti kuwekwa ili kudumisha umbali miongoni mwa watu, watoto na vijana wengi walikosa fursa za kujiendeleza. Wakati wa janga hilo walikosa uchangamfu wa kimwili, kiakili na kijamii ambao kwa kawaida wangepata wakiwa nyumbani kwa kuhudhuria shughuli za kimichezo. Ripoti za utafiti zimeonesha kwamba janga la sasa limekuwa na athari mbaya kwa ukuaji wa kimwili na kiakili kwa vijana.

Pia kumekuwapo na ongezeko la matukio yya unyanyasaji wa watoto kwa sababu familia zimelazimika kukaa nyumbani. Huku familia nyingi zikiwa na matatizo ya kifedha, watoto na vijana walikumbwa na hali mbaya ya ukosefu wa makazi na chakula ambapo wengine walitelekezwa na familia kukumbwa na mizozo ya kinyumbani. Licha ya watoto kulazimika kukaa nyumbani, masuala ambayo mara nyingi huibuliwa kwa kuwafuatilia watoto katika mazingira tofauti kama vile shule, kliniki au katika shughuli za michezo hayakufaulu, kwa sababu visa vingi vya dhuluma havikuripotiwa.

Katika kujaribu kushughulikia kutengwa na hitaji la kuwaweka watoto na vijana katika shughuli za mazoezi kwa ajili ya afya na maendeleo yao, mashirika mengi ya michezo yalipendelea mawasiliano ya mtandaoni badala ya mawasiliano ya moja kwa moja, na kusababisha hatari kubwa kwa watoto na vijana mtandaoni.

Kuendana na masharti ya janga hili kumesababisha shughuli za kijamii na michezo kufanywa kwa kuzingatia umbali miongoni mwa washiriki, licha ya kutokuwa bora kwa ukuaji wa watoto na vijana, angalau zilitoa kiwango fulani cha utangamano wa kijamii na kuwawezesha kuendelea kuwa wachangamfu kimwili na kiakili.

Janga hili lilitoa fursa kwa mashirika ya spoti na michezo kuangalia upya sera na mikakati yao ya ulinzi kwa kufanya tathmini ya hatari iliyoreboreshwa kwa mbinu mpya walizokuwa wakitumia ili kudumisha utangamano na walengwa wao na kuwahimiza kuendelea kufanya mazoezi na kutangamana (rejelea sehemu inayojadili jinsi mashirika yanaweza kutathmini hatari).

Wawezeshaji walihitaji mafunzo ya ziada kuhusu jinsi ya kutambua ishara za unyanyasaji katika mawasiliano ya mbali na watoto wakiwa mbali na watoto na vijana katika shughuli zao, uimarishaji wa kanuni za kuripoti na matumizi ya rasilimali za mtandao katika kuwasiliana na watoto na vijana katika shughuli (rejelea sehemu inayojadili jinsi wawezeshaji wanaweza kudhibiti mazoezi ya mtandaoni na usasa).

WAWEZESHAJI

Katika sehemu hii ya nyenzo, tunazingatia majukumu ya wawezeshaji, walimu, wakufunzi, washauri, viongozi wa rika, wahamasishaji n. k, wanaotoa elimu ya viungo, mazoezi, michezo au shughuli za Michezo kwa Maendeleo kwa washiriki na kutoa miongozo bora ya mazoezi kwa kuwasaidia katika kutimiza wajibu wao wa malezi.

Wawezeshaji wote wa Spoti na Michezo kwa Maendeleo, wafanyakazi na watu wanaojitolea wana wajibu wa kuwatunza watoto na watu wazima walio hatarini, na wajibu wa kuhakikisha wanaweza kushiriki katika michezo na shughuli nyinginezo katika mazingira salama, jumuishi na ya kufurahisha. Yafuatayo ni baadhi ya mambo ambayo mwezeshaji anaweza kufanya:

- kuwalinda watoto na watu wazima walio hatarini dhidi ya madhara.
- kuthibitisha wana uwezo wa kufanya kazi wakiwa na watoto au watu wazima walio hatarini kuafikia mahitaji ya mchujio.
- kuzingatia ulinzi wa kanuni za maadili.
- fanya mafunzo ya mara kwa mara kuhusu ulinzi.
- kuwa na uwezo wa kutambua ishara za dhuluma.
- kuwa na uwezo wa kushughukulikia ufichuzi.
- kujua jinsi ya kuripoti masuala yanayoibuka.
- kujenga mazingira salama ya kimichezo, jumuishi na ya kufurahisha kwa washiriki wote.

Wawezeshaji wote wanapaswa kuchangia katika desturi ya ulinzi unaopaswa kuwapa katika mashirika yote ya spoti na Michezo kwa Maendeleo. Wanapaswa kujiandikisha kwa sera ya ulinzi wa shirika na kanuni za maadili, kisha kupata mafunzo ya ulinzi wa watoto na watu wazima walio hatarini, wanajue jinsi ya kushughulikia masuala yoyote yanayohusu ulinzi na kuonesha desturi nzuri katika kufanya kazi na watoto, vijana na watu wazima walio hatarini.

Wawezeshaji wanafaa kufanya kazi ili kuhakikisha mazingira ya michezo ni salama, jumuishi na ya kufurahisha kwa watoto na watu wazima. Wanapaswa kushughulikia masuala yoyote ya mazoezi ya kishirika ambayo yanaruhusu desturi mbaya kwani hali hii inaweza kusababisha “kuchochea” ukiukaji wa mipaka unaoruhusu unyanyasaji kufanyika. Mashirika ambayo hueleza bayana kuhusu mipaka ya kutangamana na kuwafanya wawezeshaji kuzingatia desturi nzuri katika majukumu yao huwezesha mchezo salama, jumuishi na wa kufurahisha kufanyika kwa washiriki, bila madhara yasiyo ya kiajali.

Kutambua Ishara ya Dhuluma

Kama mtu mzima anayefanya kazi mara kwa mara na watoto au watu wazima walio hatarini, mwezeshaji yuko katika nafasi nzuri ya kutambua ishara za dhuluma na kuwa na jukumu la kuripoti masuala yoyote aliyo nayo. Wawezeshaji wanaweza kuanza kuwa na wasiwasi kuhusu ukuaji na usalama wa watoto, vijana au watu wazima walio hatarini baada ya kugundua ishara hizo kwa muda. Hali ya mwezeshaji kuwa na shaka tu inatosha kwake kuripoti kwa kituo

cha ulinzi au mamlaka za kisheria. Wawezeshaji hawafai kuchunguza mambo wanayoshuku, wanafaa tu kuyaripoti kwa mtu anayefaa.

Matatizo yanaweza kutokea iwapo wawezeshaji watajichunguzia wenyewe, au kufichuliwa siri na mshiriki au mtu mwingine. Iwapo ni wewe umegundua jambo na unahisi ni baya, ni bora zaidi ukishughulikia jambo hilo.

Wawezeshaji hawafai kuamua iwapo ni dhuluma iliyotokea ama la kwa sababu ni jukumu la mtu aliyeteuliwa kuchunguza masuala hayo. Wakati wa kuripoti mashaka ya dhuluma ya mtoto au mtu mzima aliye hatarini, wanaharakati wa kufichua kwa kawaida hulindwa iwapo mradi ripoti zao si za kuudhi.

Katika hali zote, usiri ni muhimu zaidi na ndiyo sababu jina la mwanaharakati wa kufichua litatambulika tu kwa mhusika iwapo atahitajika kuwa shahidi katika kesi za uhalifu au kinidhamu.

Zifuatazo ni ishara za kuonesha kuna uwezekano kwamba mtoto au mtu mzima aliye hatarini anadhulumiwa. Kuna uwezekano wa ishara hizo kukosa kuwawezesha kutambua dhuluma, hivyo ni muhimu kueleza ili kuwaridhisha. Kuna uwezekano

kwamba mtoto aliye na jeraha au mkwaruzo wa kukatwa alikuwa akicheza juu ya mti na kuanguka, hivyo kupata majeraha. Hata hivyo, matukio ya majeraha ya mara kwa mara kama haya yanaweza, kuanza kuongeza wasiwasi fulani. Haipaswi kudhaniwa kwamba ni rahisi kutambua unyanyasaji na kwamba kuna uwezekano kwa watoto na watu wazima walio hatarini kujeruhiwa kwa urahisi katika maisha ya kila siku wanaposhiriki katika shughuli mbalimbali. Wanaweza kuwa na hisia mbalimbali na zisizotabirika, hasa wakati wa ujana, au hali ya kubadilisha mienendo kwa sababu ya mambo ya nje.

Ishara mbalimbali za dhuluma:

- majeraha yasiyoelezeka kama ya moto, mikwaruzo na majeraha ya kukatwa
- maelezo tata kuhusu majeraha
- kuzungumza kuhusu vitendo vya kingono au matumizi ya lugha chafu
- kujamiiana kati ya watoto wengine au kuonesha tabia au ujuzi wa ngono kama watu wazima
- kutumia vinyago au vitu kwa mbinu za kingono
- mabadiliko katika mienendo ya kawaida, mwonekano, mtazamo au mahusiano na wengine
- mabadiliko katika ufanisi na maendeleo
- kujitenga au kutegemea sana
- mabadiliko ya haiba
- kuwa na wasiwasi kuliko awali
- kurejelea tabia za ujana
- hofu isiyoelezeka kuhusu maeneo au watu

- hofu kubwa ya kufanya makosa
- ugumu wa kutangamana
- uzito wa mwili kupungua ghafla, au kuwa na tatizo la ulaji
- kuwa msiri au kusitasita kushiriki nawe mambo

Hata hivyo, kila moja ya haya inaweza kuwa sehemu ya ukuaji wa kawaida wa mtoto. Lakini ukiona mtoto akionyesha mojawapo ya ishara hizi, inaweza kuwa ni ishara ya jambo zito zaidi na unapaswa kuwasiliana na kituo chako cha ulinzi.

Wawezeshaji wanaweza pia kuchunguza mienendo ya watu wazima kwa watoto au watu wazima walio hatarini, ambayo inazua wasiwasi, kama vile mawasiliano yasiyofaa katika mitandao ya kijamii, kutoa lifti au zawadi, upendeleo na mikutano ya siri. Haya ni masuala yanayowezekeka ambayo yanapaswa kuangaziwa na kituo cha ulinzi katika shirika..

Kushughulikia Ufichuzi

Kutokana na stadi za maisha zinazofundishwa kupitia shughuli za Spoti na Michezo kwa Maendeleo, pamoja na kupata maelezo kuhusu haki zao na jinsi ya kuzitumia, watoto na watu wazima walio hatarini hujenga hulka ya kutafuta usaidizi, kama vile kuzungumza na mtu mzima wanayemwamini katika mitandao yao wakihisi kutokuwa salama. Kwa kuwa ni mtu mzima anayeaminika, mtoto au mtu mzima aliye hatarini anaweza kujisikia huru kumwambia mwezeshaji iwapo unyanyaswa.

Watoto na watu wazima walio hatarini wanaweza kushindwa kufichua matatizo yao. Inaweza kuwa vigumu sana kufichua dhuluma katika baadhi ya vikundi - watoto kutoka makabila tofauti wanaweza kushindwa kuwapata watu wa kuwaeleza siri zao, kunaweza kuwa na vizuizi vya lugha, au mtoto au mtu mzima anaweza kushindwa kujieleza kwa sababu ya ulemavu.

Ikiwa mtoto au mtu mzima aliye hatarini anaonesha kwamba anadhuriwa, au taarifa inapokelewa ambayo inaibuta wasiwasi kwamba mtoto au mtu mzima aliye hatarini anadhuriwa, mwezeshaji anayepokea taarifa hiyo anapaswa::

1. **kutulia** na kuhakikisha kwamba mtoto au mtu mzima yuko huru na anahisi salama.
2. **kusikiliza kwa makini** kile kinachosemwa, kuruhusu mtoto au mtu mzima kujieleza kwa kasi chake wenyewe.
3. kufafanua kwamba kuna uwezekano kwamba **taarifa itashirikiwa kwa wengine** – usijaribu kuahidi kutunza siri, lakini eleza kwamba ni wale tu ambao wanafaa kujua ili kusaidia kuwalinda ndio watakaofahamishwa. Desturi nzuri ni kuomba idhini kutoka kwa mtoto, hata kama hauhitaji kushiriki habari hiyo.
4. **fupisha maswali** kuhakikisha ujumbe ni rahisi kueleweka na sahihi kwa yote yanayosemwa. Epuka maswali ya kumpeleleza mtu huyo kwa taarifa zaidi kuliko anavyotoa.
5. **mhakikishie** mtoto au mtu mzima kwamba amefanya jambo zuri katika kushiriki maelezo.
6. dhihirisha na umwambie mtoto au mtu mzima kwamba anachosema **kitachukuliwa kwa**

uzito na utambue ugumu wowote uliopo katika kuelewa alichokisema.

7. mwambie mtoto au mtu mzima **kitakachofanyika baadaye** na mwenigine atayefahamishwa habari.
8. **rekodi kwa maandishi** yote yaliyosemwa ikiwezekana, tumia maneno ya mtoto au mtu mzima.

Rekodi tarehe na wakati, majina yoyote yaliyotajwa na yule aliyepewa taarifa hiyo. Taarifa inapaswa kuandikwa jinsi ilivyotolewa, na kubainisha kile kinachozingatiwa kama ukweli, tetesi au maoni, ambapo rekodi inapaswa kuwekwa saine na tarehe.

Wawezeshaji wanaopewa taarifa wanaweza kupata hisia kama vile mshtuko, hasira au kuhisi kushindwa. Ni muhimu kuficha hisia hizi kwa sababu zinaweza kumwathiri vibaya mhusika ambaye ni mtoto au mtu mzima aliye hatarini.

Ni muhimu kuwa mtulivu, kutoa usaidizi na kuelekeza suala hilo kwenye kituo cha ulinzi kilichoteuliwa au, elekeza kwa polisi au afisa wa huduma za kijamii ikiwa mtoto au mtu mzima aliye hatarini yuko katika hatari ya dharura.

Hupaswi kamwe kupuuza tatizo, bila kujali kama unaamini kile unachoambiwa au la. Unafaa kuripoti ufichuzi wakati wote – ufichuzi wa uvumi, hata wakati mtu hajulikani, japo ni nadra. Unaweza pia kuwa na jukumu la lazima kisheria kuripoti tatizo hilo kwa polisi au afisa wa huduma za kijamii.

Ni muhimu kutowasiliana na mshukiwa kwa sababu hii inaweza kumweka mtoto au mtu mzima aliye hatarini

katika hatari zaidi au kuhitilafiana na uchunguzi wa uhalifu. Unafaa pia kuepuka kufanya uchunguzi wa kibinafsi kuhusu tukio au kutoa maoni mabaya kuhusu mtuhumiwa.

Ni wajibu wa mwezeshaji kuripoti ufichuzi, SI kuuchunguza.

Kuripoti Mashaka

Mashirika ya Spoti na Michezo kwa Maendeleo yanapaswa kuwa na taratibu za kimsingi za kuripoti masuala ya unyanyasaji. Malalamishi yanaweza kujumuisha hali ambapo madhara yanatokea katika shirika au nyumbani ama kwingineko katika jamii. Mashaka yanaweza kuwa ya sasa au kuhusu hali ya zamani (tukio la awali za dhuluma). Yanaweza kuwa mashaka kuhusu kuhangaishwa (unyanyasaji, dhuluma, kupuuza au ukandaizaji), desturi mbaya au shirika kushindwa kuwalinda watoto au watu wazima walio hatarini.

Bila kujali mahitaji ya kisheria kuhusu ulazima wa kuripoti, ni desturi nzuri kuripoti, matukio ya dhuluma yanayoshukiwa kwa mamlaka husika ili kuchunguzwa. Hata hivyo, wawezeshaji wanapaswa kufahamu, kwamba kuna mahitaji ya lazima ambayo yanawalazimu kuripoti wasiwasi wa madai ya unyanyasaji wa watoto au watu wazima walio hatarini kwa polisi na mamlaka ya huduma za kijamii katika nchi mbalimbali, na kutofanya hivyo kunaweza kusababisha kushtakiwa.

Ikiwa mtoto au mtu mzima aliye hatarini yuko katika hatari ya haraka ya madhara makubwa, wasiwasi

unapaswa kuripotiwa kwa polisi na/au ofisi ya huduma za kijamii. Fuatilia ripoti hiyo kwa kuwasiliana na mhusika wako anayeshughulikia ulinzi.

Ikiwa mtoto au mtu mzima aliye hatarini hayuko katika hatari ya moja kwa moja au ikiwa suala hilo ni ukiukaji wa kanuni za maadili au ni desturi mbaya, basi ripoti suala hilo kwa kiongozi wako. Ikiwa shirika lako halijateua kiongozi maalumu wa ulinzi, tatizo linaweza kuripotiwa kwa mtu yeyote mkuu zaidi katika shirika au jamii yako.

Hakikisha kwamba watu wanaohitaji kufahamishwa kuhusu jambo hilo ni wale wanaotaka kusaidia kumlinda mtoto au watu wazima walio hatarini kukabiliwa na madhara.

Malalamishi yanaweza kuripotiwa:

- Kwa maandishi tumia fomu ya kuripoti malalamishi katika shirika lako au, hata bila fomu, kwenye karatasi iliyotiwa saine na tarehe.
- Kwa simu au barua pepe kwa polisi, ofisi ya huduma za kijamii au kiongozi maalum wa ulinzi.
- Ana kwa ana kwa polisi, ofisi ya huduma za kijamii au kiongozi maalum wa ulinzi.

Ni desturi zuri kuhakikisha kuwa nambari za mawasiliano au anwani za kuripoti zimetolewa kwenye kadi au kwenye vitabu/vifaa vinavyotolewa kwa wawezeshaji, wafanyakazi na viongozi wa shirika.

Mienendo Salama

Shughuli za Spoti na Michezo kwa Maendeleo zinalenga kukuza vipaji vya michezo na stadi za maisha za washiriki wao, si kukuza mchezaji kiufundi tu bali pia kiujumla. Muhimu zaidi katika mpango huu ni mwezesaji, ambaye lazima awe na uhusiano bora na endelevu na washiriki.

Wawezeshaji wanahitaji kuwasiliana na washiriki kwa njia nzuri na kuzingatia umri, jinsia na uwezo, uhamasishaji, sifa na maoni chanya. Ni muhimu waheshimu mitazamo tofauti, wajumuishe na wajenge hali ya kuwakubali washiriki wote. Kwa kuboresha shughuli ili kukidhi mahitaji ya washiriki wote, wawezeshaji watawafanya kufurahia ushiriki wenye ufanisi.

Kupitia mafunzo bora ya mienendo na kudumisha mazingira salama kwa washiriki wote, shughuli za Michezo kwa Maendeleo zinaweza kuleta matokeo chanya kwa washiriki wote.

Ili kuunda mazingira salama ya michezo, mashirika ya Spoti na Michezo kwa Maendeleo yanahitaji kuzingatia hatari ya washiriki kuweza kukabiliwa na unyanyasaji, dhuluma, kutelekezwa au ukandamizaji na mikakati ya kupunguza hatari hizi. Katika sura inayofuata tunajadili mbinu kutathmini hatari na mikakati ya kupunguza hatari. Katika sura hii tutajadili baadhi ya maeneo na shughuli hatarishi, pamoja na wawezeshaji na utekazi wao.

Kituo cha Mazoezi

Wawezeshaji wanafaa kutambua hatari zinazotokana na kituo kinachotumika kwa shughuli za shirika. Je, kituo kiko salama au wananchi wanaingia ndani wakati wowote? Je, kituo kinatumiwa na vikundi vingine? Je, washiriki wako wanaelekezwa kila wakati? Je, kuna watu wenye kamera wanaopiga picha au video za washiriki? Nini hufanyika iwapo mshiriki anahitaji kwenda msalani? Je, vyumba vya kubadilishia nguo, bafu na vyoo vinatumiwa na makundi mengi au ni vya kikundi hiki cha mafunzo pekee?

Haya ni maswali muhimu ya kujuliza, lakini muhimu vilevile ni kuweka mikakati ya kukabili hatari kama hizo.

Vyumba vya Kubadilisha, Mabafu, Vyumba vya Huduma ya Kwanza

Vyumba vya kubadilishia nguo, mabafu na vyumba vya huduma ya kwanza ni maeneo hatarishi ambapo mikakati inafaa kuwekwa ili kuhakikisha usalama wa washiriki. Mashirika yanapaswa kuwa na sera, au sheria, zinazohusu matumizi ya vyumba vya kubadilishia nguo, mabafu na vyumba vya huduma ya kwanza. Pale ambapo shirika linafanya kazi katika kituo cha umma au cha pamoja, sera ya vyumba vya kubadilishia nguo, vyoo na vyumba vya huduma ya kwanza inafaa kubuniwa kwa ushirikiano na mwenye kituo.

Wakati mwingine, vyumba tofauti vya kubadilishia nguo, vinapaswa kutengwa kwa ajili ya wanaume na wanawake, isipokuwa pale ambapo kuna upungufu wa vituo, katika hali hiyo ifahamike wazi kwamba

mtu hafai kuingia katika vyumba vya kubadilishia nguo ambavyo vinatumiwa na watu wa jinsia tofauti.

Watu wazima hawapaswi kuruhusiwa kubadilishia nguo katika chumba kimoja wakati mna watoto. Simu za rununu zisitumike kwenye vyumba vya kubadilishia nguo ili kuepuka kurekodi video au kupiga picha.

Wasiwasi wowote au matukio yanayofanyika katika kituo cha kubadilishia nguo, choo au chumba cha huduma ya kwanza lazima yaripotiwe bila kuchelewa.

Mtu mzima anafaa kusimama nje ya vyumba vya kubadilishia nguo na kuwapa watoto muda wa kubadilishia. Kwa kusimama nje, watoto wanaweza kuripoti kwa watu wazima kwa urahisi ikiwa wanahisi kutokuwa salama na mtu mzima anaweza kuwa hapo ili kuzuia udhalilishaji.

Iwapo mashirika hayawezi kutoa vyumba salama vya kubadilishia nguo, washiriki wote wanafaa kushauriwa kufika wakiwa wamevalia mavazi yao ya mafunzo ya michezo ndani ya nguo zao au trakisuti.

Mashirika yanaweza kumweka afisa wa klabu nje ya milango ya chumba cha kubadilishia nguo, jambo ambalo huwawezesha watoto kutafuta usaidizi wanapohitaji.

Sajili ya Mahudhurio

Wawezeshaji wanapaswa kuweka rekodi ya mahudhurio ya vipindi vyote vya mafunzo wanayofanya. Ikiwa mtoto, kijana au mtu mzima aliye hatarini atapotea, hii itasaidia kutoa taarifa za kuwapata. Sajili itumike kuonesha mshiriki anapoingia ndani na kutoka nje ya kikao.

Sajili za mahudhurio zinapaswa kuhifadhiwa kwa usalama, na data iliyomo inafaa kudhibitiwa kwa njia inayozingatia sheria ya ulinzi wa data.

Safari ya Mbali na Nyumbani

Matukio ya urafiki wa kupumbaza na dhuluma za kijinsia katika michezo mara nyingi huhusishwa na vipindi vya muda ambavyo washiriki husafiri mbali na nyumbani kuhudhuria kambi za mafunzo, mashindano au hafla.

Watoto, vijana na watu wazima walio hatarini wako katika hatari kubwa ya kusafirishwa kwenda katika maeneo, miji au hata nchi nyingine, hivyo mashirika, wawezeshaji na wazazi wanapaswa kukagua ipasavyo mialiko ya kusafiri kutoka nyumbani hadi kwenye kambi namashindano ili kuhakikisha si njama za shughuli za ulanguzi wa binadamu.

Shughuli zote zinazohusisha safari za mbali na nyumbani, zinafaa kufanyiwa tathmini ya hatari na kuwekwa mikakati ya ulinzi. Ngazi zinazofaa za usimamizi zinapaswa kuwekwa kwa kuzingatia mahitaji ya watoto au watu wazima walio hatarini ambao wanahudhuria. Vikundi vilivyochanganywa vinapaswa kuwa na waangalizi wa kiume na wa kike. Mipango ya malazi inapaswa kuzingatia masharti ya jinsia tofauti na kuepuka watu wazima kulala katika vyumba sawa na watoto. Rekodi inafaa kuwekwa kila wakati ili kuhakikisha hakuna mtoto au mchezaji anayepotea.

Uwiano wa Watu wazima na Watoto

Wawezeshaji wanapaswa kufahamu uwiano unaopendekezwa wa watu wazima kwa watoto katika michezo wanayofundisha. Pia wanapaswa kuangalia kama sheria au miongozo ya serikali katika nchi yao ina uwiano wa usimamizi uliopendekezwa kitaifa. Ikiwa hakuna mwongozo mahususi kuhusu hili katika nchi yao, uwiano ufuatao wa watu wazima kwa watoto unapendekezwa ili kusaidia kuwalinda watoto:

- unapofanya shughuli na watoto kati ya umri wa miaka sita na minane, uwiano wa juu wa mtu mzima kwa watoto ni 16 na unapaswa kuzingatiwa.
- unapofanya shughuli na watoto kati ya umri wa miaka sita na minane, uwiano wa juu wa mtu mzima kwa watoto ni 20 na unapaswa kuzingatiwa.

Ikiwa wanafunzi wakubwa wanasaidia kuwaelekeza watoto wadogo, ni wale tu wenye umri wa miaka 18 au zaidi wanapaswa kujumuishwa kama watu

wazima wakati wa kuhesabu uwiano wa watu wazima kwa watoto. Shughuli zote zinazopangwa kila wakati zinafaa kuwahusisha angalau watu wazima wawili. Hii ni desturi nzuri inayopendekezwa ya ulinzi. Angalia Kanuni ya Uwili hapa chini.

Mambo yafuatayo yanapaswa pia kuzingatiwa katika kuamua ni watu wazima wangapi wanaohitajika kuwaelekeza watoto kwa usalama:

Mambo yafuatayo yanapaswa pia kuzingatiwa katika kuamua ni watu wazima wangapi wanaohitajika kuwaelekeza watoto kwa usalama:

- idadi ya watoto wanaohusika katika shughuli hiyo.
- umri, jinsia, ukomavu na viwango vya uzoefu wa watoto.
- iwapo mmoja wa wafanyakazi, watu wa kujitolea au watoto wana ulemavu wa kujifunza au kimwili au mahitaji maalum.
- iwe kuna mmoja wa watoto ambaye ana mienendo ya usumbufu.
- hatari zinazohusiana na shughuli.
- hatari zinazohusiana na mazingira.
- kiwango cha uwezo na uzoefu wa wawezeshaji.
- ratiba kamili ya shughuli.

Kumbusho Muhimu

- Hakikisha kuna angalau mtu mzima mmoja kwa kila kundi la watoto wa jinsia moja na watoto wanaohusika.
- Hakikisha kuna angalau mtu mzima mmoja wa kila jinsia katika makundi yenye mchanganyiko.
- Katika shughuli zote zinazopangwa kila wakati angalau watu wazima wawili wanafaa kuhusishwa. Pasipowezekana kuwa na wawezeshaji wawili, waombe wazazi au walezi kuhudhuria kikao kama waangalizi.
- Watu wazima hawafai kuachwa na watoto peke yao.
- Watu wote wazima wanaokutana na watoto moja kwa moja wanapofanya kazi wanafaa kufanyiwa mchujo na lazima watie saini kanuni za maadili kisha wawe wamemaliza mafunzo ya uhamasisho wa ulinzi.

Kanuni ya Uwili

Kanuni ya Uwili³ ni mwongozo wa desturi nzuri wakati wa kufanya kazi na watoto au watu wazima walio hatarini. Kimsingi, mwezeshaji hafai hata mara moja kuwa peke yake na mtoto mmoja au watu wazima walio hatarini anapofanya kazi pamoja nao.



3 Chama cha Makocho wa Kanada - Hatua Tatu za Ufundishaji Bora - <https://coach.ca/three-steps-responsible-coaching>

Wawezeshaji wanafaa kuepuka kugusa sehemu zote za nyeti za mwili – sehemu za uzazi, makalio au matiti. Iwapo mgusano wa bahati mbaya utatokea wakati wa kumshika mshiriki, mwezeshaji anafaa kuomba msamaha na kurekodi tukio hilo kwa maandishi kuwajulisha wazazi/walezi na kiongozi wa ulinzi. Vitendo kama vile kupiga kofi makalio ya mshiriki kama ishara ya pongezi haviruhusiwi kabisa.

Desturi ya Mtandao na Mawasiliano ya Kidijitali

Mawasiliano ya aina yote kwa kutumia njia zilizo hapo juu yanapaswa kupitia kwa wazazi/walezi wao.

Kwa kutegemea idhini ya wazazi, wawezeshaji wanaweza kuwasiliana na vijana walio na umri wa zaidi ya miaka 16 ama kwa barua pepe/maandishi ya kikundi au kwa kunakili barua kwa kiongozi wa ulinzi aliyeteuliwa na shirika pamoja na wazazi/walezi. Wawezeshaji wanafaa kuacha mawasiliano yawe ya mafunzo au masuala ya shirika na hawapaswi kufanya mawasiliano ya kibinafsi mtandaoni na watoto au watu wazima walio hatarini.

Katika tukio ambapo mtoto amemwoneesha mwezeshaji ujumbe wa SMS, picha au barua pepe ambayo haifai kwa mtoto kuwa nayo, mwezeshaji kwa wakati huo lazima amjulishe kiongozi wa ulinzi aliyeteuliwa na shirika.

Kadiri teknolojia inavyoendelea, intaneti na huduma zake mbalimbali zinaweza kufikiwa zaidi kupitia vifaa mbalimbali kama vile simu za rununu, runinga mahiri, kompyuta na mitambo ya michezo. Ingawa mtandao unatumika kwa mambo mengi mazuri, hutoa jukwaa la usambazaji wa picha za dhuluma za watoto na uhalifu wa kimtandao. Aidha, tovuti za mitandao na majukwa ya mazungumzo mtandaoni yameendelea kutumiwa na watu kwa madhumuni ya 'urafiki wa kupumbaza' watoto na watu wazima walio hatarini kwa njama ya kudhulumu, na hutumiwa kwa watoto na vijana kama jinsi ya kudhalilisha.

Figure 4: Kanuni 3 za Kudhibiti Usalama wa Mtandao⁴



4 Ufahamu wa Watoto, Usalama wa Binafsi na Wajibu wa Teknolojia, https://www.kidsintheknow.ca/app/en/about-role_of_technology

Mtoto akikutumia ombi la kutaka kukuongeza kama rafiki kwenye mitandao ya kijamii, unafaa kukataa ombi hilo iwapo huna idhini ya mzazi (au mlezi). Pia hupaswi kukubali ombi lake la urafiki ikiwa unatumia akaunti yako ya mitandao ya kijamii kwa madhumuni ya kibinafsi na kuna uwezekano kwamba akaunti yako inaweza kujumuisha picha au maudhui ambayo hayafai au yatachukuliwa kuwa yasiyo ya kitaalamu kwa mtoto au kijana kuyatazama au kuyasoma. Inaweza kukuondolea hadhi ya kitaaluma

Kurekodi Video/Upigaji picha

Watu wengi wanaweza kupiga picha au kurekodi video na kuzisambaza siku hizi kwa urahisi kutokana na simu mahiri na mtandao. Kunaweza kuwa na sababu nyingi nzuri za kuchukua na kusambaza picha na video za washiriki katika shughuli za Spoti na Michezo kwa Maendeleo, lakini pia unahitaji kufahamu kuna hatari za matumizi ya picha na video zinazofaa kutiliwa maanani. Ulinzi wa data na ulinzi wa haki za mtu anayehusika unapaswa kuzingatiwa.

Mara nyingi picha za washiriki hutumiwa kukuza na kusherehekea shughuli, matukio na mashindano. Washiriki na wazazi/walezi hutaka kutumia fursa za kusherehekea au kutangaza kuhusika na mafanikio yao katika shughuli za spoti na Michezo kwa Maendeleo kwa kutumia picha na kurekodi video. Wawezeshaji pia huona ni bora kutumia picha au video wakati wa mafunzo ya mazoezi.

Ili kuepuka matumizi yasiyofaa kwa picha au rekodi za video za wachezaji, tunafaa kuweka ulinzi wa kudhibiti:

- matumizi, kubadilisha au kuhariri picha kwa madhumuni ya kuwanyanyasa au kuwadhulumu washiriki wa mchezo au juhudi za kuwatambulisha kwa watu ili kunyanyaswa au kudhulumiwa.
- matumizi ya picha kwa lengo la unyanyasaji wa watoto, au kubadilisha na kuhariri kwa madhumuni haya.

- uwezekano wa mtoto kutambuliwa kutokana na taarifa za kibinafsi na urafiki wa kupumbaza ambao unaweza kufuatia baadaye.
- uwezekano wa watoto kutambulika kuwa hatarini kwa sababu kama vile:
 - kutengwa kutoka familia zao kwa ajili ya usalama wao wa binafsi.
 - vikwazo vya upatikanaji wa wazazi baada ya wazazi kutengana.
 - kuwa shahidi katika kesi za kisheria.

Ni lazima tutambue kwamba picha na video kwenye tovuti na mitandao ya kijamii, na katika mabango, vyombo vya habari au machapisho mengine zinaweza kutumiwa vibaya na kusababisha hatari za moja kwa moja ama zisizo za moja kwa moja kwa watoto au watu wazima walio hatarini. Washiriki wanaweza kujipata katika urafiki wa kupumbazwa, unyanyaswa, dhuluma au kudhalilishwa kwa sababu ya picha iliyorekodiwa kwenye kifaa chochote.

Mashirika ya Spoti na Michezo kwa Maendeleo yanapaswa kuwa na sehemu ya upigaji picha na kurekodi video katika sera zao za ulinzi. Sera hiyo inaweza kupiga marufuku kurekodi picha za washiriki au kuweka masharti kwa mtu yeyote anayerekodi picha za washiriki kujiandikisha kwanza katika shirika au kutia saini kwenye fomu ya idhini.

Kunapaswa kuwa na marufuku ya kurekodi picha za aina yoyote katika vyumba vya kubadilishia nguo, mabafu na maeneo ya huduma ya kwanza.

Kunapaswa kuwa na marufuku ya kurekodi picha za aina yoyote katika vyumba vya kubadilishia nguo, mabafu na maeneo ya huduma ya kwanza.

Ikiwa picha ya mtoto aliye chini ya umri wa miaka 18 itachapishwa au kutumiwa na shirika kwa sababu

yoyote ile, idhini inahitajika kutoka kwa wazazi/walezi wao. Wazazi/walezi wanaweza kukataa kuruhusu watoto wao kupigwa picha au kurekodiwa video, na hii haifai kutumiwa kumtenga mtoto katika shughuli zozote.

Umakinifu unafaa kuzingatiwa wakati wa kutumia picha zozote zinazoonesha watoto au watu wazima walio hatarini kwenye tovuti ya shirika, mitandao ya kijamii au katika machapisho mengine. Picha za matukio zinafaa kuonesha kusudio la shughuli za michezo huku zikilinda heshima ya washiriki. Picha za watoto au watu wazima walio hatarini wakiwa wamevalia mavazi au seti pekee ndizo zinazofaa kutumika. Picha au video zinazoonekana kuwa na utata zinafaa kuepukwa kwani zinaweza kutumiwa vibaya na watu wengine katika mazingira tofauti. Picha zinapaswa kuzingatia tukio na ikiwezekana, ziwe za kikundi badala ya kumwonesha mtu binafsi.

Michezo inaweza kutoa fursa ya uwezekano mkubwa wa matumizi mabaya ya picha au video, kwa hivyo picha zinafaa:

- kuepuka kuonesha uso na mwili halisi wa mtoto au mtu mzima aliye hatarini – badala yake, waoneshe kutoka kwenye kiuno au mabega kwenda juu.
- kuepuka picha na pande za kamera ambazo zinaweza kuchochea tafsiri potofu au matumizi mabaya kuliko nyingine.

Wazazi/walezi wanafaa kuonywa kwamba kunaweza kuwa na matokeo mabaya kwa kusambaza picha zinazohusishwa na taarifa za watoto wao au watoto wa watu wengine kwenye mitandao ya kijamii (kwa mfano, Facebook, Twitter, Instagram au njia zozote za mitandao ya kijamii) – na tahadhari inafaa kuhusu ‘utambulishaji’.

Ikiwa shirika linahifadhi na kutumia picha ili kuwatambua watoto au watu wazima kwa madhumuni rasmi, kama vile vitambulisho, basi linafaa kuhakikisha linazingatia mahitaji ya kisheria ya kushughulikia taarifa za binafsi, yaani, sheria ya ulinzi wa data.

JAMII

Mashirika ya Spoti na Michezo kwa Maendeleo yanaweza kufanya kazi na washiriki wanaohudhuria shughuli zao na jamii kwa ujumla kuhusu mikakati ya na kanuni za ulinzi. Kwa vile ni jukumu la kila mtu kuwalinda watoto, vijana na watu wazima walio hatarini, shughuli zinafaa kuwahusisha wengi zaidi kuliko shirika pekee, wafanyakazi wake na watu wanaojitolea pekee. Wanajamii wanahitaji kushirikishwa katika ulinzi, wakiwamo watoto na watu wazima walio hatarini ambao wanashiriki katika mpango huo na wazazi/walezi wao na wanajamii wengine.

Mashirika ya Spoti na Michezo kwa Maendeleo yanaweza kujihusisha katika ngazi ya kijamii kwa:

- kuanzisha mpango wa Michezo kwa Maendeleo wenye mbinu ya kufundisha stadi za maisha kupitia mchezo wa mafunzo ya mbinu za usalama wa binafsi kwa washiriki. Kwa mfano, kuwahamisha kuhusu haki zao na jinsi ya kujilinda.
- kuwahusisha washiriki na wanajamii wengine katika kufanya tathmini ya hatari na kupanga mipango ya kupunguza madhara yanayohusiana na ulinzi, kwa mfano, jinsi ya kutumia desturi salama wakati wa kwenda na kuondoka uwanjani.
- kwa kutumia eneo au ramani ya jamii kama njia ya kuwafundisha washiriki kuhusu sehemu zenye madhara makubwa dhidi ya maeneo salama ambapo wanaweza kupata msaada.

Mbinu za Usalama wa Binafsi

Mbinu za Usalama wa Binafsi ni stadi za maisha zinazolenga kuzuia watoto au watu wazima walio hatarini kuwa waathiriwa wa unyanyasaji, dhuluma au kutelekezwa.

Mashirika mengi ya Michezo kwa Maendeleo hufundisha stadi za maisha kupitia michezo ambayo ipo katika nafasi nzuri ya kufundisha mbinu za usalama wa binafsi kwa watoto na watu wazima walio hatarini. Stadi za maisha ni mchanganyiko wa ujuzi wa binafsi, wa uhusiano wa mtu na watu na wa utambuzi, vilevile ufahamu na mtazamo.

Uhusiano wa Mtu na Watu,
Uhusiano wa Mtu wa Watu,
na Mbinu za Utambuzi
(anachomiliki mtu)



Ufahamu
(anachojua mtu)



Stadi za Maisha au Umilisi
(anachoweza mtu kufanya)



Mtazamo au Mienendo
(anachoamini na kuthamini mtu)

Mbinu za Usalama wa Kibinafsi wakati mwingine hujulikana kama mienendo ya kujilinda. Zinaeleza kile ambacho mtu anaweza kufanya ili kujilinda kutokana na unyanyasaji, dhuluma au kutelekezwa. Mbinu hizi zinafaa kufundishwa kwa njia inayolingana na umri lakini inaweza kuanza mapema kama miaka minne. **Watoto wadogo hawapaswi kufichuliwa habari kuhusu unyanyasaji wa kingono kwa watoto, lakini wapewe habari kuhusu usalama wa kibinafsi.**

Ni muhimu kutambua kwamba ni watu wazima ambao wana jukumu la utunzaji kuhakikisha watoto wako salama. Watoto hawapaswi kuachiwa jukumu la kujilinda wao wenyewe. Sababu muhimu ya kufundisha mienendo ya kujilinda ni kuhakikisha watoto na vijana wanajua haki zao na wametambua watu wazima wanaoaminika maishani mwao ambao wanaweza kuwatafuta wakiwa na wasiwasi au wakihisi kuwa hatarini.

Jedwali lifuatalo linaonesha mtalaa unaopendekezwa kulingana na vikundi vinne vya umri wa watoto na vijana:

Miaka 4-7	Miaka 7-11	Miaka 11-14	Miaka 14-18
<ul style="list-style-type: none"> • Hisia za Kibinafsi • Mfumo wa Mtandao Salama • Sawa na Si Sawa • Siri • Idhini • Sehemu za Siri • Udhalilishaji • Mtandao Salama 	<ul style="list-style-type: none"> • Ufanisi wa kibinafsi • Mfumo wa Mtandao Salama • Afya bora na Afya duni • Mahusiano • Siri • Idhini • Masuala ya Ngono na Uzazi • Afya na Haki • Udhalilishaji na Ubaguzi • Mtandao Salama 	<ul style="list-style-type: none"> • Ufanisi wa kibinafsi • Hitaji la Msaada • Afya bora na Afya duni • Mahusiano • Siri • Idhini • Masuala ya Ngono na Uzazi • Afya ya uzazi • Afya na Haki • Udhalilishaji na Ubaguzi • Ubaguzi 	<ul style="list-style-type: none"> • Ufanisi wa kibinafsi • Mfumo wa Mtandao Salama • Afya bora na Afya duni • Mahusiano • Siri • Idhini • Masuala ya Ngono na Uzazi • Afya na Haki • Udhalilishaji na Ubaguzi • Mtandao Salama

Madhumuni ya kufundisha mbinu za usalama wa binafsi ni kuimarisha uwezo wa kustahimili wa watoto na vijana wanapokua na kusitawi, kutoa stadi muhimu za maisha ili kuwalinda kutokana na hali za dhuluma na kuwasaidia kuepuka hali mbalimbali zinazoweza kuwa hatari. Mbinu za usalama wa kibinafsi zinashughulikia haki ya kijana kuhisi na kuwa salama na kuwafanya kuwa na uwezo wa kutathmini na kutenda ipasavyo katika hali ambazo ni salama na hatari.

Watoto na vijana hujifunza stadi muhimu za kuwasaidia kukabiliana na hali zinazoweza kuwa hatari kwa njia ambayo huimarisha usalama wao wa kibinafsi. Pia ni vigumu kwa wahalifu kuwalenga waathiriwa ambao wana wanaonesha kuwa na mbinu za usalama wa kibinafsi.

Shughuli za Michezo kwa Maendeleo huwawezesha watoto kuwa na mijadala iliyo wazi kutafakari na kufikiria kwa kina kuhusu usalama wao binafsi. Kutokana na mijadala ya shughuli za michezo, wanaweza kujifahamisha kuhusu usalama, ustawi wao na mikakati iliyopo ya ulinzi.

Mijadala kama hiyo inaweza kusaidia zaidi katika kufichua masuala ya wasiwasi kuhusu ulinzi. Watoto na vijana wanapaswa kufahamishwa kuhusu taratibu za kueleza wasiwasi wao au kutoa ripoti na jinsi ripoti yoyote itakavyoshughulikiwa. Hatua hiyo ijumuishe michakato ya wakati wana wasiwasi unaomhusu rafiki au mwanarika. Wawezeshaji wanapaswa kufahamu jinsi ya kuwasaidia watoto na jinsi ya kushughulikia ripoti ya ulinzi kutoka kwa mtoto au kijana.

Matokeo ya Mafunzo ya Usalama wa Kibinafsi

Jedwali lifuatalo⁵ linaweka bayana baadhi ya mambo ambayo watoto na vijana wanapaswa kufanya kuhusiana na usalama wa kibinafsi katika umri au hatua tofauti za ukuaji wao.



MIAKA 4-7

HATUA YA 1 (MIAKA 4-7)

WATOTO WANAFAA KUJIFUNZA.....

Hisia za Kibinafsi	<ul style="list-style-type: none"> kutambua na kubainisha hisia zao, kutofautisha kati ya hisia nzuri na mbaya. kuamini silika zao na kumwambia mtu anapohisi kuwa hatarini. mbinu za kimsingi za kupinga shinikizo la kufanya jambo wasilotaka, na ambalo linaweza kuwafanya wawe hatarini. ni bora kusema “la” kwa kitu au mtu ambaye huwafanya wahisi kuchanganyikiwa au kuwa na wasiwasi. kutambua njia ambazo wao ni sawa na tofauti kwa wengine. jinsi ya kuwasikiliza watu wengine, kucheza na kufanya kazi kwa ushirikiano. jinsi ya kuzungumza na kutoa maoni kuhusu mambo ambayo ni muhimu kwao.
Mfumo wa Mtandao Salama	<ul style="list-style-type: none"> kuwatambua watu wazima wanaoaminika katika maisha yao na jinsi ya kupata usaidizi kutoka kwao. wanachofaa kufanya iwapo wanahisi kuwa hatarini au wasiwasi wao wenyewe au wengine; nani wa kuomba msaada na msamiati wa kutumia wakati wa kuomba msaada; umuhimu wa kuendelea kujaribu kuomba msaada mpaka wasikilizwe. jinsi ya kujibu vizuri kwa watu wazima ambao hawaelewi.
Sawa na Si Sawa	<ul style="list-style-type: none"> about what is kind and unkind behaviour, and how this can affect others. about how to treat themselves and others with respect; how to be polite and courteous. about how to respond if physical contact makes them feel uncomfortable or unsafe.
Siri	<ul style="list-style-type: none"> tofauti kati ya siri ambazo ni vyema kuweka (kwa mfano, sherehe ya kushtukiza) na siri ambazo zinafaa kufichuliwa kwa mtu mzima anayeaminika (kwa mfano, siri kuhusu mguzo wa kimwili au upigaji picha).
Idhini	<ul style="list-style-type: none"> kujua kuhusu hali na wakati wanapaswa kuomba ruhusa, vilevile wakati idhini yao inaweza kuhitajika.

⁵ Matokeo ya kujifunza yameelezwa na mitalaa mbalimbali inayoshughulikia usalama wa kibinafsi ukiwamo Mpango wa Kusoma kwa Elimu ya PHSE unaopatikana katika <https://www.pshe-association.org.uk/curriculum-and-resources/resources/programme-study-pshe-elimu-muhimu-hatua-1%E2%80%9335>



MIAKA 4-7

Sehemu za Siri

- kujua kuhusu hali na wakati wanapaswa kuomba ruhusa, vilevile wakati idhini yao inaweza kuhitajika.
- majina sahihi ya sehemu za mwili, ikijumuisha sehemu gani za mwili ambazo ni za siri na hazipaswi kuguswa au kuonekana kwa wengine, kwamba sehemu za mwili wao zilizofunikwa na nguo za ndani ni za siri.
- umuhimu wa faragha wakati wa kubadilisha nguo, kuoga na kwenda msalani.

Uchokozi

- kwamba mili na hisia zinaweza kuumizwa kwa maneno na vitendo; kwamba watu wanaweza kusema maneno ya kuumiza mambo.
- kuhusu jinsi watu wanaweza kuhisi wakikumbana na mienendo ya kuumiza au kudhalilisha.
- tabia hiyo ya kuumiza kama vile kudhihaki, kuitana majina, kudhalilisha na kuwagua wengine kwa makusudi haikubaliki; jinsi ya kuripoti unyanyasaji; umuhimu wa kumwambia mtu mzima anayeaminika.

Mtandao Salama

- kuhusu kazi ya mtandao katika maisha ya kila siku.
- kuhusu jinsi mtandao na vifaa vya kidijitali vinaweza kutumiwa kwa usalama kutafuta mambo na kuwasiliana na wengine.
- kwamba wakati mwingine watu wanaweza kuwa na tabia tofauti mtandaoni, kama vile kuficha utambulisho wao.
- kwamba habari zote zinazoonekana mtandaoni si za kweli.




MIAKA 7-11

HATUA YA 2 (MIAKA 7-11)

WATOTO WANAFAA KUJIFUNZA.....

Ufanisi wa Kibinafsi	<ul style="list-style-type: none"> jinsi ya kubashiri, kutathmini na kudhibiti hatari katika hali mbalimbali. vishawishi vya mara kwa mara ambavyo watu hutumia wanapotaka kuwadhuru au kuwakandamiza vijana. jinsi ya kutambua shinikizo kutoka kwa wengine kufanya jambo hatari au linalowaletea wasiwasi na mikakati ya kudhibiti hali hii. kuhusu haki za binadamu ambazo zipo kumlinda kila mtu na uhusiano kati ya haki na wajibu. jinsi ya kujibu vyema na ipasavyo kwa watu wazima ambao wanaweza kukutana nao (katika mazingira mbalimbali, ikiwamo mtandaoni) na ambao hawawafahamu.
Mtandao wa Usalama	<ul style="list-style-type: none"> wapi pa kupata ushauri na kuripoti matukio iwapo kuna wasiwasi kuhusu usalama wao wenyewe au wa mtu mwingine (pamoja na mtandaoni). kuwajua watu wazima wanaoaminika katika mfuo wao wa mtandao usalama.
Mahusiano mazuri/ Mahusiano Yasiyofaa na Yasiyo Mazuri	<ul style="list-style-type: none"> kutambua kwamba kuna aina mbalimbali za mahusiano (km, urafiki, mahusiano ya kifamilia, mahusiano ya kimapenzi, mahusiano ya mtandaoni). kwamba watu wanaweza kuvutiwa na mtu fulani kihisia, kimapenzi na kingono; kwamba watu wanaweza kuvutiwa na mtu wa jinsia moja au jinsia tofauti kwao; kwamba utambulisho wa jinsia na mwelekeo wa kijinsia ni tofauti. kwamba kulazimisha mtu yeyote kuoa kinyume na matakwa yake ni hatia; kwamba msaada na usaidizi unapatikana kwa watu ambao wana wasiwasi kuhusu hali hiyo kwa wao wenyewe au wengine. kwamba watu wanaopendana na kujaliana wanaweza kuwa katika uhusiano wa kujitolea (kwa mfano, ndoa) na kuishi pamoja lakini pia wanaweza kuishi mbali. mikakati ya kutambua na kudhibiti ushawishi wa wanarika na hamu ya kukubaliwa na wanarika katika urafiki; kutambua athari za vitendo vya mtandaoni kwa wengine. kutambua ikiwa urafiki (mtandaoni au nje ya mtandao) unawafanya wahisi kuwa hatarini au wasiwasi; jinsi ya kushughulikia hali hii na kuomba msaada iwapo unahitajika.
Siri	<ul style="list-style-type: none"> kuhusu kutunza siri au usiri, wakati gani unapaswa (km, kushutukiza siku ya kuzaliwa ambayo wengine watajua) au haifai kukubaliwa, na wakati upi bora wa kuvunja usiri au kusambaza siri.
Idhini	<ul style="list-style-type: none"> kuhusu kutafuta na kutoa idhini (kibali) katika hali mbalimbali. kuhusu usiri na mipaka ya kibinafsi, ni nini kinafaa katika urafiki na mahusiano kwa jumla (pamoja na mtandaoni). kutambua aina mbalimbali za mguso wa kimwili; ni nini kinachokubalika na kisichokubalika; mikakati ya kukabiliana na kesi za mguso usiotakikana kimwili.



MIAKA 7-11

Masuala ya ngono na Uzazi Uzazi Afya na Haki

- kutambua sehemu nyeti za nje na viungo vya ndani vya uzazi kwa wanaume na wanawake na jinsi gani mchakato wa kubalehe unahusiana na uzazi wa kibinadamu.
- kuhusu mabadiliko ya kimwili na kihisia yanayofanyika wakati wa kukaribia na kupitia kubalehe (pamoja na hedhi, ukweli muhimu kuhusu mzunguko wa hedhi na ukuaji mzuri wa hedhi, uume kusimama, na ndoto za ngono).
- kuhusu jinsi taratibu za usafi zinavyobadilika wakati wa kubalehe, umuhimu wa kuwa safi na jinsi ya kudumisha usafi wa kibinafsi.
- abokuhusu mchakato ya uzazi na kuzaliwa kama sehemu ya mzunguko wa maisha ya mwanadamu; jinsi mimba inavyotungwa na watoto kuzaliwa (na kwamba kuna njia za kupanga uzazi); jinsi watoto wachanga wanavyohitaji kutunzwa.
- kwamba ukeketaji (FGM) ni ukiukaji wa haki za binadamu, nini cha kufanya na nani wa kumwambia iwapo wanadhani wao au mtu wanayemjua anaweza kuwa hatarini.

Udhalilishaji

- kuhusu athari za udhalilishaji (nje ya mtandao na mtandaoni) na madhara ya mienendo ya kuumiza.
- mikakati ya kukabiliana na mienendo ya kuumiza inayoshuhudiwa au kuonwa, nje ya mtandao na mtandaoni (ikiwa ni pamoja na kudhihaki, kutusi, udhalilishaji, kuchamba, kunyanyaswa au kubaguliwa wengine kimakusudi); jinsi ya kuripoti wasiwasi na kupata msaada.
- kuhusu ubaguzi: maana yake na jinsi ya kuukabili.

Mtandao Salama

- kuhusu umuhimu wa kuweka taarifa za binafsi kuwa za siri; mikakati ya kuweka usalama mtandaoni, ikijumuisha jinsi ya kudhibiti maombi ya maelezo ya kibinafsi au picha zao wenyewe na wengine; hatua ya kuchukua iwapo wanaogopa au wana wasiwasi na kitu kinachoonekana au kusoma mtandaoni na jinsi ya kuripoti wasiwasi, masuala yasiyokubalika na mawasiliano.
- kuhusu kwa nini mtu anaweza kuwa na tabia tofauti mtandaoni, ikiwa ni pamoja na kujidai kuwa mtu mwingine ambaye siye; mikakati ya kutambua hatari, mudhui na mtagusano hatari; jinsi ya kuripoti wasiwasi.
- kutambua njia ambazo intaneti na mitandao ya kijamii inaweza kutumika vizuri na vibaya.
- jinsi ya kutathmini uaminifu wa vyanzo vya habari mtandaoni; na jinsi ya kufanya chaguo salama, la kuaminika kutoka kwenye matokeo ya utafutaji.
- kutambua mambo yanayofaa kusambazwa na mambo ambayo hayafai kusambazwa kwenye mitandao ya kijamii; kanuni za kudhibiti usambazaji wa picha.



MIAKA 11-14

HATUA YA 3 (MIAKA 11-14)

Watoto wanafaa kujifunza.....

Ufanisi wa kibinafsi	<ul style="list-style-type: none"> mikakati rahisi ya kusaidia kujenga ustahimilivu kwa maoni hasi, maamuzi na maoni. jinsi ya kutambua madhara na kudhibiti usalama wa kibinafsi katika hali zinazozidi kuwa huru, ikiwa ni pamoja na mtandaoni, ili kuchukua hatua kulingana na hisia zako. njia za kutathmini na kupunguza madhara yanayohusiana na afya, ukuaji na usalama wa kibinafsi. jinsi ya kubashiri, kutathmini na kudhibiti hatari katika hali mbalimbali.
Kuhitaji Msaada	<ul style="list-style-type: none"> wapi pa kupata msaada, ni watu wazima gani ambao wanaaminika katika maisha yao ambao wanaweza kutafutwa kwa ushauri na usaidizi, ni mashirika gani ambayo yana mazingira bora kwa watoto ambayo yanafanya kazi katika jamii yao na yanayoweza kutoa ushauri na usaidizi kuhusu afya na usalama wa umma.
Mahusiano mazuri na Mahusiano Yasiyofaa na Yasiyo Mazuri	<ul style="list-style-type: none"> viashiria bora vya mahusiano mazuri na mahusiano yasiyofaa, kwa kujumuisha mtandaoni. kubainisha na kukuza maadili ya kibinafsi katika urafiki, mapenzi na uhusiano wa kimapenzi. umuhimu wa uaminifu katika mahusiano na mienendo inayoweza kudhoofisha au kujenga uaminifu. kutathmini matarajio kuhusu majukumu ya kijinsia, mienendo na urafiki katika mahusiano ya kimapenzi. kudhibiti hisia kali zinazoweza kutokana na mahusiano (ikiwa ni pamoja na mvuto wa kingono) kwamba kila mtu ana chaguo la kuchelewesha ngono, au kufurahia urafiki bila ngono. jinsi ya kuunda, kudumisha na kudhibiti mahusiano mazuri, yakiwamo ya mtandaoni, kwa usalama na uaminifu. sifa na mienendo ambayo wanapaswa kutarajia na kuzionesha katika aina mbalimbali za mahusiano mazuri (kama vile shuleni na jamii kwa jumla, familia na urafiki, ikiwa ni pamoja na mtandaoni).
Siri	<ul style="list-style-type: none"> kuhusu kutunza siri au faragha, wakati gani unapaswa kukubaliwa (km, kushutukiza siku ya kuzaliwa ambayo wengine watajua) au haifai kukubaliwa, na wakati upi bora wa kuvunja usiri au kusambaza siri.



MIAKA 11-14

Idhini	<ul style="list-style-type: none"> kuhusu sheria inayohusiana na idhini ya masuala ya ngono. jinsi ya kutafuta, kutoa, kutotoa na kuondoa idhini katika mazingira mbalimbali, kama vile mtandaoni. kwamba anayeomba idhini anawajibika kisheria na kimaadili kuhakikisha kwamba kibali hicho kimetolewa; kwamba ikiwa idhini haijatolewa au kuondolewa, uamuzi huo unafaa kuheshimiwa kila wakati. athari za kusambaza picha za ngono za watu wengine bila idhini.
Afya ya Uzazi na Haki	<ul style="list-style-type: none"> mikakati ya kudhibiti mabadiliko ya kimwili na kiakili ambayo ni sehemu ya kawaida ya kukua, ikiwa ni pamoja na kubalehe na ukuaji wa hali ya hedhi. madhara yanayohusu ngono isiyo salama. matokeo ya mimba zisizopangiwa, vyanzo vya usaidizi na chaguzi zinazopatikana kwamba baadhi ya maambukizi yanaweza kuenezwa kwa njia ya ngono na kwamba vizuizi vya mpango wa uzazi huleta ulinzi dhidi ya baadhi ya magonjwa ya zinaa, pamoja na VVU. kuhusu malengo, umuhimu na mbinu mbalimbali za kupanga uzazi; mbinu na sehemu za kupata huduma na ushauri kuhusu mpango wa uzazi. ujuzi wa mawasiliano na mazungumzo unaohitajika kwa matumizi ya uzazi wa mpango katika mahusiano mazuri tofauti kati ya jinsia ya kibayolojia, utambulisho wa kijinsia na mwelekeo wa kijinsia. kutambua kwamba mvuto wa kingono na kujamiiana ni tofauti. kwamba ndoa ni ahadi ya kisheria, kijamii na kihisia ambayo wanandoa wanafaa kujiingiza kwa uhuru, na kamwe bila mtu kulazimishwa kwa vitisho au kushurutishwa. kupima utayari wa kujamiiana. kwamba uhusiano wa karibu unafaa kuwa wa kufurahisha. hatari na imani potofu zinazohu ukeketaji wa wanawake, hali yake kuwa kitendo cha uhalifu na mikakati ya kupata usaidizi kwa usalama wao wenyewe au wengine ambao wanaweza kuwa katika hatari, au ambao tayari wamefanyiwa ukeketaji.



MIAKA 11-14

Udhalilishaji na Ubaguzi

- sifa za miendendo ya unyanyasaji, kama vile urafiki wa kupumbaza, unyanyasaji wa kijinsia, kingono na unyanyasaji wa kihisia, ukatili na ukandamizaji; kutambua ishara za tahadhari, ikiwa ni pamoja na mtandaoni; jinsi ya kuripoti mienendo ya unyanyasaji au kupata usaidizi wao wenyewe au kwa wengine.
- kutambua ushawishi wa wanarika na kuweka mikakati ya kuudhibiti, ikijumuisha mtandaoni.
- jukumu ambalo wanarika wanaweza kufanya katika kusaidiana ili kupinga shinikizo na ushawishi, kupinga desturi mbaya ya mitandao ya kijamii na kupata usaidizi ufaao.
- kwamba hitaji la kukubalika na mwanarika linaweza kuleta hisia za shinikizo na kuzidisha kufanya maamuzi yenye madhara; mikakati ya kukabili hali hii.
- kuhusu kufananisha, tofauti, na utofauti kati ya watu wa rangi mbalimbali, tamaduni tofauti, uwezo, jinsia, utambulisho wa kijinsia, umri na mwelekeo wa kijinsia.

Mtandao Salama

- mikakati ya kutambua na kupunguza madhara kutoka kwa watu mtandaoni ambao tayari hawawafahamu, ni lini na jinsi gani ya kupata usaidizi.
- kwamba vipengele vya mtandao vinaweza kuongeza madhara na fursa, kwa mfano, kasi na ukubwa wa kusambaza habari, mipaka ya umma na ya binafsi isiyoonekana na mtazamo wa kutokujulikana.
- kuweka maadili ya binafsi na kuweka wazi mipaka katika nyanja za maisha ambazo wanataka zibaki kuwa siri; mikakati ya kudhibiti kwa usalama taarifa za kibinafsi na picha mtandaoni, ikiwemo kwenye mitandao ya kijamii.
- manufaa na matumizi chanya ya mitandao ya kijamii, ikijumuisha jinsi inavyoweza kutoa fursa ya kujihusisha na mitazamo mbalimbali kuhusu masuala mbalimbali.
- kuelewa jinsi watu wanavyojieleza mtandaoni kunaweza kuwaletea athari nzuri na mbaya.
- kufanya maamuzi bora ya iwapo mambo tofautitofauti yaliyomo katika vyombo vya habari na mitandao ya kijamii yanafaa kutizamwa kisha ubuni mbinu za kuyashughulikia.
- kushughulikia ipasavyo mambo yanapoharibika mtandaoni, ikiwa ni pamoja na kutafuta msaada kwa ujasiri, kutoa taarifa kwa mamlaka na majukwaa mengine.
- jinsi ya kudhibiti ombi lolote au shinikizo la kusambaza picha yao wenyewe au ya wengine, na jinsi ya kutafuta msaada.



MIAKA 14-18

HATUA YA 4 (MIAKA 14-18)

Vijana wajifunze....

Ufanisi wa Binafsi

- mikakati ya kukuza ujasiri na kujenga uwezo wa kustahimili ushawishi wa wanarika na ushawishi mwingine unaoathiri jinsi wanavyojifikiria wao wenyewe na afya na ukuaji wao.
- mikakati ya kutambua hali za madhara na dharura, ikiwa ni pamoja na mtandaoni; njia za kudhibiti haya na jinsi ya kupata usaidizi ufaao, ikijumuisha pale ambapo kunaweza kuwa na madhara ya kisheria (kwa mfano, dawa za kulevya na pombe, uhalifu wa kutumia nguvu na majambazi).

Hitaji la Msaada

- kutathmini na kudhibiti madhara na usalama wa binafsi katika mazingira mbalimbali, ikiwamo mtandaoni; kuhusu usaidizi uliopo wa kuwalinda katika mazingira haya na jinsi ya kupata usaidizi huo.
- jinsi ya kutambua, na kutafuta msaada katika tukio la, unyanyasaji wa kijinsia, ukandamizaji, kujeruhiwa au ubakaji, na mchakato wa kuripoti tukio kwa mamlaka husika.

Mahusiano Mazuri na Yasiyo Mazuri

- sifa na manufaa ya mahusiano thabiti na mazuri, pamoja na msaada wa pande zote, uaminifu, heshima na usawa.
- jukumu la furaha katika mahusiano ya karibu, ikiwa ni pamoja na kupata mshindo kimapenzi.
- kushughulikia ipasavyo viashiria vya mahusiano yasiyofaa, ikiwa ni pamoja na kutafuta msaada pale panapofaa.
- kuhusu kutofautiana katika mvuto wa kimapenzi na kingono na kuendeleza ujinsia, ikiwa ni pamoja na vyanzo vya msaada na kutiwa moyo na jinsi ya kuvipata.
- mikakati ya kupata ushauri na usaidizi unaofaa, sahihi na ufaao na mahusiano, na kuwasaidia wengine kuupata unapohitajika.
- mikakati ya kudhibiti hisia kali zinazohusu hatua tofauti za mahusiano.
- kudhibiti mabadiliko vizuri na kwa uwajibikaji katika mahusiano ya binafsi, ikiwa ni pamoja na kutamatisha mahusiano.
- mbinu za kukabili huzuni mahusiano yanapobadilika, ikiwa ni pamoja na athari za kutengana, talaka na kufiwa; vyanzo vya msaada na jinsi ya kuvipata.
- kutumia mashauriano ya kujenga mahusiano na kukubaliana kuhusu suluhu ya matatizo.
- kudhibiti mwisho wa mahusiano vizuri na kwa heshima, ikijumuisha mtandaoni.
- kutambua fursa za kujenga mahusiano yenye umuhimu mahali pa kazi na mipaka inayozunguka mahusiano ya kitaaluma.



MIAKA 14-18

- jinsi ya kubainisha maadili katika uhusiano wao na kuyatumia katika aina mbalimbali za mahusiano.
- kudhibiti urafiki uliokomaa, ikijumuisha kupata marafiki katika maeneo mapya.
- kutambua kufuatiliwa kusikofaa (kama vile unyanyasaji na unyemeleaji ikiwa ni pamoja na mtandaoni), njia za kushughulikia na jinsi ya kutafuta msaada.
- kuhusu athari za mienendo inayohusu unyanyasaji wa kijinsia na kupinga kulaumiwa kwa waathiriwa, ikiwa ni pamoja na unyanyasaji unapotokea mtandaoni.
- kubainisha athari za dawa za kulevyo na pombe kwenye uteuzi na mienendo ya kingono.
- mbinu za kutathmini utayari wao kwenye ngono, ikiwa ni pamoja na shughuli za masuala ya ngono mtandaoni, kama mtu binafsi na kati ya wanandoa.
- kutathmini hali inayochochea na mazingira mbalimbali ambapo picha za ngono zinasambazwa, na matokeo yanayowezekana kisheria, kihisia na kijamii.
- kutambua wakati wengine wanatumia hila, ushawishi, au kulazimisha na jinsi ya kushughulikia.
- sheria inayohusiana na unyanyasaji katika mahusiano, ikiwa ni pamoja na udhibiti wa vitisho na unyanyasaji wa mtandaoni.
- kutambua wakati uhusiano ni wa dhuluma na mikakati ya kudhibiti hali.
- ujuzi na mikakati ya kukabili ukandamizaji, udhalilishaji, unyanyasaji na udhibiti wa mahusiano.
- kuhusu changamoto zinazokumba upatikanaji wa msaada katika hali mbalimbali za dhuluma za kinyumbani; umuhimu wa kufanya hivyo; vyanzo vya ushauri na usaidizi ufaao, na jinsi ya kupata msaada huo.
- sheria inayohusiana na ukatili wa 'kuheshimu' na ndoa za lazima; matokeo kwa watu binafsi na jamii pana na njia za kupata usaidizi.

Siri

- kuhusu kutunza siri au faragha, wakati gani unapaswa kukubaliwa (km, kushutukiza siku ya kuzaliwa ambayo wengine watajua) au haifai kukubaliwa, na wakati upi bora wa kuvunja usiri au kusambaza siri.

Idhini

- kuelewa majukumu ya kimaadili na kisheria ambayo mtu anayeomba kibali anayo, na umuhimu wa kuheshimu na kulinda haki ya watu kutoa, kutotoa au kutoa idhini yao (katika mazingira mbalimbali, pamoja na mtandaoni).
- kuelewa matokeo ya kihisia, kimwili, kijamii na kisheria iwapo utashindwa kuheshimu haki ya wengine kutotoa au kuondoa idhini.



MIAKA 14-18

Sexual Health and Relationships

- aina mbalimbali za uhusiano wa karibu — ikiwa ni pamoja na mtandaoni — na uwezo wao wa kihisia na madhara ya kimwili (zote nzuri na mbaya).
- kuhusu magonjwa ya zinaa ikiwa ni pamoja na VVU, matibabu na jinsi ya kupunguza madhara ya maambukizi.
- jinsi ya kufanya iwapo mtu ana, au anaweza kuwa na magonjwa ya zinaa (pamoja na njia za kupata huduma za afya ya uzazi).
- kukabili viziwi, (ikiwa ni pamoja na aibu, uvumi, na imani potofu) kuhusu afya ya uzazi na matumizi ya huduma za afya ya uzazi.
- kuhusu mimba yenye afya na jinsi chaguo la mtindo wa maisha linavyoathiri mtoto anayekua tumboni.
- kwamba hali ya uzazi inaweza kutofautiana kwa watu wote, hubadilika kwa wakati (pamoja na kikomo cha hedhi) na wanaweza kuwa wameathiriwa na magonjwa ya zinaa na mambo mengine ya mtindo wa maisha.
- kuhusu uwezekano wa mimba kuharibika na usaidizi unaopatikana kwa watu ambao hawawezi kubeba au kudumisha ujauzito.
- kuhusu chaguo na usaidizi unaopatikana katika tukio la mimba isiyopangiwa, na jinsi ya kupata msaada na ushauri ufaao.
- kuelewa madhara ya mimba zisizopangiwa na ushauri kwa wazazi wachanga; kwa kutambua manufaa ya kuchelewesha mimba, huku ukikubali mabadiliko katika hali ya uzazi na umri.
- kukubaliana na mpenzi wako, na ikibidi kuwa na uwezo wa kupendekeza, matumizi ya mpango wa uzazi.
- kukuza ufahamu wa kina wa jinsi ya kuchagua mpango wa uzazi unaofaa katika mazingira na mahusiano mbalimbali.
- jinsi ya kupunguza madhara ya kuambukizwa au kuambukiza magonjwa ya zinaa.
- jinsi ya kuwajibika kwa afya zao ya uzazi na kujua wapi, na jinsi gani, ya kupata ushauri wa karibu, utambuzi wa magonjwa na matibabu.
- jinsi ya kutumia vyema mbinu tofauti tofauti za kudhibiti mimba, ikijumuisha jinsi na mahali pa kupata huduma hizo.
- kutathmini njia zinazofaa zaidi za kuzuia mimba katika hali mbalimbali (ikiwa ni pamoja na mbinu za dharura za kuzuia uzazi).
- kufikia mbinu mbalimbali zinazopatikana katika tukio la mimba isiyotarajiwa na kuelewa umuhimu wa kupata ushauri na usaidizi wa dharura.
- kukuza na kudumisha mahusiano yenye afya, yenye kupendeza na kuchunguza viwango tofauti vya urafiki wa kihisia.
- kutathmini viwango tofauti vya urafiki wa kihisia katika mahusiano, jukumu la furaha, jinsi wanavyoelewa tofauti kati ya 'mapenzi' na 'tamaa ya kujamiiana'.



MIAKA 14-18

Uchokozi na Ubaguzi

- mikakati ya kupinga aina zote za maoni ya kuumiza na ubaguzi.
- kutathmini jinsi mienendo yao inaweza kuwashawishi wenzao, kwa uzuri na ubaya, ikijumuisha mtandaoni, na katika hali zinazohusisha silaha au magenge.
- ujuzi wa kuwasaidia vijana wanarika wakiwa katika nafasi za ushawishi.
- kutambua hali ambazo wanaathiriwa vibaya, au wako katika hatari, kutokana na uhusiano wao na kikundi fulani au magenge; mikakati ya kupata usaidizi ufaao.
- kutambua udhalilishaji na unyanyasaji mahali pa kazi kwa namna zote na njia za kutafuta au kutoa msaada wa kushughulikia hali hiyo.
- kutambua na kudhibiti msukumo mbaya, udanganyifu, na ushawishi katika mazingira mbalimbali, ikiwa ni pamoja na mtandaoni.
- mikakati ya kutambua, kudhibiti na kuepokana na hali hatari za kijamii.
- kutathmini hatari na madhara ya kujihusisha na majambazi, uhalifu mkubwa wa kupangwa au kubeba silaha.
- kutambua na kupinga maoni ya kuumiza na ubaguzi, na kuelewa haki na majukumu ya ujumuishaji.
- kutambua, kuheshimu na, kama inafaa, kupinga jinsi imani au mitazamo mbalimbali ya kitamaduni inavyoathiri uhusiano.
- njia za kuenzi tamaduni mbalimbali, kukuza ujumuishaji na kwa busara upinge maoni ya kuumiza pamoja na ubaguzi.

Mtandao Salama

- majukumu ya kisheria na kimaadili ambayo watu wanayo kuhusiana na mitazamo mbalimbali kuhusu mahusiano mtandaoni.
- kuweka na kudumisha mipaka kuhusu faragha ya kibinafsi na kudhibiti usalama mtandaoni katika njia zote, kukiwamo kutafuta msaada unapofaa.
- kupinga kwa nguvu mambo yaliyomo mtandaoni ambayo yanawaathiri vibaya wao binafsi au kuharibu sifa zao za kitaaluma.
- kujenga na kudumisha uwepo mzuri wa kitaalumu mtandaoni, kwa kutumia teknolojia mbalimbali.
- jinsi mitandao ya kijamii inaweza kupanua, kuweka mipaka au kupotosha mitazamo na kutambua jinsi mambo wanayoyaunda na kusambaza yanaweza kuchangia au kupinga hili.
- kuwa mtumiaji wa kuchuja taarifa za mtandaoni katika aina zake zote, ikiwa ni pamoja na kutambua upendeleo, propaganda, na udanganyifu.
- kudhibiti usalama wa kibinafsi katika mahusiano mapya, ikijumuisha shughuli za mtandaoni au wakati wa kukutana na mtu ambaye walipatana mtandaoni kwa mara ya kwanza.
- kuelewa athari zinazoweza kusababishwa na maonesho ya masuala ya ngono katika ponografia na maudhui mengine.

Mbinu za Kijamii za Kukabili Hali za Kimichezo

Mbinu bora ya kuwahusisha washiriki na wanajamii wengine katika kufanya tathmini za hatari na kupanga mikakati ya kupunguza madhara yake katika ulinzi ni Mbinu ya Kuzuia Hali kwa mujibu wa Kaufman⁶. Imechukuliwa kutoka kwenye mfumo wa kuzuia uhalifu, Mbinu ya Kuzuia Hali ya Kaufman iliyoungwa kwa ajili ya mashirika yanayowahudumia vijana.

Lengo la kutumia Mbinu ya Kuzuia Hali ya Kaufman ni kutambua masuala mengi yanayohusiana na hatari inayowezekana katika mazingira ya shirika la Spoti na Michezo kwa Maendeleo katika kipindi fulani maalumu. Mbinu hii inahimiza kutambua aina mbalimbali za hatari zinazoweza kusababisha maelfu ya matokeo mabaya tofauti (kwa mfano, dhuluma za kijinsia, unyanyasaji wa kimwili, majeraha yasiyokusudiwa, matatizo ya kiafya, uonevu).

Dhana mbili muhimu za mbinu hii jumuiishi. Kwanza, hali moja ya hatari inaweza kusababisha matokeo mbalimbali mabaya (kwa mfano, usimamizi duni unaweza kusababisha dhuluma za kingono kwa watoto, au vijana kujihusisha na mienendo hatari inayosababisha jeraha bila kukusudia, au kwa mtoto mkubwa kumdhulumu mdogo). Pili, mbinu jumuiishi iliyokusudiwa kutambua na kutatua hatari zote zinazowezekana katika mpangilio wa shirika ndiyo njia pekee ya kuhakikisha usalama wa vijana.

Mbinu ya Kuzuia Hali ya Kaufman ina hatua nne:

1. Jopo kazi linalojumuisha wafanyakazi, watu wa kujitolea, washiriki, wazazi/walezi na wanajamii linabuniwa ili kujadili hatari za ulinzi katika shirika.
2. Baada ya kutambua hatari, basi jopokazi hutambua suluhu ya kivitendo na inayofaa zaidi katika kushughulikia kila hatari iliyotambuliwa (inapowezekana, mikakati ya kuzuia hupendelewa kuliko mikakati ya kupunguza hatari na msisitizo huwekwa kwenye matumizi ya uwezo na nyenzo za ulinzi).
3. Kisha timu ya usimamizi wa shirika inaorodhesha hatari za kushughulikiwa kwa kuzingatia nyenzo zilizo (kwa mfano, uzito wa yanayoweza kutokana na suala, gharama ya suluhisho).
4. Mpango rahisi wa utekelezaji wa ulinzi unafanywa kisha kutumika kuongoza mchakato wa kupata suluhisho.

Mbinu ya Kuzuia Hali ya Kaufman huzingatia sehemu zifuatazo kama utaratibu wa mikutano ya jopokazi linalojadili hatari za ulinzi:

1. **Maeneo yenye hatari kubwa** ndani ya shirika mpangilio (kwa mfano, madarasa yasiyotumika, maghala).
2. **Hali ya watoto au watu wazima walio hatarini** (kwa mfano, watoto kutoka familia maskini, watu wazima wenye matatizo ya kujifunza) ambayo huongeza hatari.
3. **Mambo ambayo yanaweza kuleta “kuvutia”** madhara mengine (kwa mfano, uwiano duni wa wafanyakazi/watu wa kujitolea kwa washiriki, wafanyakazi wa muda mrefu ambao si lazima wazingatie sheria).
4. **Sera za shirika na jamii** (k.m., shughuli za uajiri, sheria za matumizi ya vifaa vya jamii au kushindwa kushughulikia dhuluma za majambazi waliopo)
5. **Mtindo wa maisha na shughuli za kila siku** za washiriki (kwa mfano, watoto wanaowasili mapema kwenye vipindi kama wazazi wapo kazini) na wafanyakazi/watu wa kujitolea (kwa mfano, wafanyakazi wanaotembea nyumbani na washiriki ambao ni vijana).
6. **Mazingira pana ya kijamii** (kwa mfano, majengo yaliyoachwa ambayo vijana huchozea ndani wakiwa njiani kwenda kwenye vikao, mitaa isiyokuwa na taa za kutosha)
7. **Matatizo ya kiafya, kukabili visa vya ajali, na masuala ya usalama wa kimwili** yanawakilisha madhara yote yanayotokana na dhuluma za kijinsia kwa watoto. Hii ni pamoja na masuala mbalimbali ambayo yanaweza kuhusishwa na kudumisha afya ya washiriki (kwa mfano, vifaa duni vya kunawia/vyumba vya usafi), kudhibiti ajali (km, kuzuia majeraha wakati wa michezo), na kuhakikisha usalama wa kimwili (kwa mfano, majeraha kutokana na mapigano, udhalilishaji, au shughuli za uhalifu).

⁶ Keith na Tews, Hayley na Schuett, Jessica na Kaufman, Benjamin. (2012). Kinga ni Bora kuliko Tiba: Thamani ya Kinga ya Hali katika Mashirika. Kubuni Mashirika Salama: Hatua za Vitendo za Kuzuia Dhuluma za Watoto kwa Wanaofanya Kazi nao. 140-169. 10.1002/9781119943228.ch8..



Urutibu wa Ramani ya Jamii

Kuunda ramani za eneo au jamii ni muhimu katika kuwasaidia washiriki kujifunza jinsi ya kukaa salama kutokana na unyanyasaji, dhuluma au kutekelezwa au katika kusaidia mashirika kupanga mikakati yao ya ulinzi.

Ramani inaweza kuwa ya jamii kwa ujumla au ya eneo maalum kama vile shule, mafunzo au ukumbi wa mashindano. Kuchora ramani kupitia mchakato shirikishi unaohusisha washiriki na wanajamii wengine ili kusaidia kutambua maeneo na watu ambao wana hatari ya madhara ya ajali au yasiyo ya ajali kwa watoto na watu wazima walio hatarini.

Ramani zinaweza kutumika kuwajulisha washiriki kuhusu maeneo na watu ambao wanaweza kuwa hatari kwao ama maeneo na watu ambao wanaweza kutoa usaidizi na kuwaweka salama.

Kwa mfano, jengo lililoachwa au eneo la biashara za pombe si mahali pazuri zaidi kwa mtoto au mtu mzima aliye hatarini kuzurura, ilhali kanisa au shule inaweza kuchukuliwa kuwa mahali salama pa kukaa.

Ramani ya jamii ambayo imechorwa na washiriki wenyewe kupitia zoezi za pamoja au na shirika inaweza kuwasaidia vijana kufanya maamuzi bora wakati wa kuamua ni wapi na nani watakayemtembelea na kukaa naye.

Kutumia ramani ya jamii kama shughuli shirikishi huruhusu watoto na watu wazima kuhusika katika ulinzi wao wenyewe. Kwa watoto hii huwapa sauti na kuheshimu haki yao ya kusikilizwa. Kifungu cha 12 cha UNCRC kinasema watoto na vijana wana haki ya kibinadamu ya kutoa maoni na maoni haya kusikilizwa

na kuchukuliwa kwa uzito. Kuwahusisha watoto, kuhimiza ushiriki wao kikamilifu, na kuwasikiliza kunakuza ufahamu wao wa haki zao, hujenga kujiamini, huongeza kujithamini, huanzisha ujuzi wa uongozi, na kuboresha ujasiri wao wa kujadiliana na watu wazima.

Kuwezesha Vikao vya Kuchora Ramani za Jamii pamoja na Watoto na Vijana


1. Wakusanye watoto au vijana katika kipindi na uaulize wanafikiri "Ramani ya Jamii" ni nini? Mwezesaji anadhibiti maoni na kudokeza kwamba ni pamoja na mahali watu wanapoishi, watu wanapoenda, maeneo tofauti na alama muhimu, maeneo ambayo ni mazuri na hatari sana, mahali ambapo unaweza kupata vitu unavyohitaji.
2. Kisha waulize watoto na vijana kufikiria kuhusu mahali wanapoishi, wanachofanya kila siku, na wale wanaowaona.
3. Wagawe watoto na vijana katika vikundi vidogo kisha kila kikundi ukipe kipande cha karatasi kubwa ya chati ya kugeuzwa na kalamu za rangi. Unaweza pia kuwapa majarida, mikasi, gundi, alama za rangi, au karatasi iwapo utataka, ambazo wanaweza kuzitumia kuboresha ramani zao.
4. Ambia kila kikundi kichore jamii yao kwenye karatasi ya chati ya kugeuzwa. Ambia kila kikundi kina dakika 30 kukamilisha kazi hiyo. Hakikisha kikundi kinajumuisha alama kuu katika jamii (mito, barabara, miti mikubwa ya mikutano) na maeneo ambayo ni muhimu kwa jamii (kituo cha mafuta, maduka,

shule, makanisa/ misikiti, maeneo ya nyumba, mabomba ya maji, migahawa, baa, masoko, makao ya polisi/wanajeshi, NGOs).

5. Kila kikundi kichora ramani, waulize watoto na vijana baadhi ya maswali ili kuwafanya wafikirie zaidi kuhusu ramani ya jamii yao. Je, ni maeneo gani muhimu katika jamii yako na kwa nini ni muhimu? Wako wapi watu ambao ni muhimu kwako, ni akina nani na wanafanya nini? Je, wewe huenda maeneo gani katika jamii na kufanya nini huko? Je, ni wapi katika jamii unajifunza mambo mapya?
6. Waambie watoto na vijana wachore nyota (*) kando ya maeneo yote ambayo ni salama katika jamii yao. Wape dakika chache kukamilisha kazi kisha waulize: "Kwa sababu gani mahali hapa ni salama? Je, ni salama kwa watoto au watu wazima wote walio hatarini? Palikuwa salama kila wakati?"
7. Baada ya dakika chache waambie watoto na vijana waweke alama ya makasi (x) kando ya sehemu zote ambazo si salama kwa watoto na watu wazima walio hatarini. Wape dakika chache kujadili na kukamilisha hili. Waulize: "Ni nini kinachofanya mahali hapa pasiwe salama? Je, si salama kwa watoto na vijana wote? Siku zote huwa si salama?"

Watoto au vijana wanaweza kuwa na maoni tofauti tofauti kuhusu kile ambacho ni salama na kisicho salama, na baadhi ya maeneo yanaweza kuwa na nyota (*) na X. Shule zinaweza kuwa salama kwa sababu zinasaidia watoto kujifunza katika mazingira yafaayo kwa watoto. Hata hivyo, baadhi ya watoto wanaweza, kuhusisha shule kuwa mahali pa udhalilishaji au dhuluma na hivyo kusema si salama.

8. Mara tu ramani zitakapokamilika, ambia kila kikundi kichore mchoro wa Venn wenye Maeneo Salama (Uwezo) katika mduara mmoja na Maeneo yasiyo Salama (Changamoto) kwenye duara jingine. Waambie washiriki kwamba maeneo ambayo ni salama na yasiyo salama yanapaswa kuwa katikati ya mchoro wa Venn chini ya mada ya tofauti. Mchoro wa Venn chini ya mada ya tofauti.



9. Kisha mwezesaji apitie ramani pamoja na watoto na vijana na kuwauliza mambo waliyoyifunza kutokana na zoezi hilo. Mwezesaji asifikirie maana ya kila ramani na anapaswa kuuliza maswali ili kuwasaidia washiriki kuelewa vyema kila ramani.

Wakati wa shughuli hakikisha watoto na vijana wote wameridhishwa na kipindi na kwamba kila mtu anashiriki katika shughuli na maoni yake kusikilizwa.

Urutibu wa Ramani ya Jamii kwa Mashirika

Urutibu wa ramani za jamii unaweza kusaidia mashirika ya Michezo kwa Maendeleo na wawezeshaji wao kutambua vyanzo vya usaidizi ndani ya jamii yao. Polisi wapo wapi na nani anahusika na masuala ya ulinzi wa mtoto? Ni mashirika gani hutoa huduma bora za kijamii na afya kwa watoto? Yanapatikana wapi?

Urutibu wa ramani za jamii mara nyingi huitwa urutibu wa ramani ya rasilimali unaozingatia jamii kwa kuwa unalenga kuunda ramani inayobainisha mali zilizopo katika jamii kama sehemu ya mchakato rasmi au usio rasmi wa kupanga jamii. Falsafa ya "msingi wa mali" ni ya kawaida katika Urutibu wa ramani za jamii ambapo hatua ya kwanza katika mchakato wa maendeleo ni kutambua uwezo na mali ya jamii, ikiwa ni pamoja na ya wakazi wake, kisha kutumia mali hizi kujenga mpango wa utekelezaji.

Kinachofanya urutibu wa ramani wa mali kuwa wa kipekee ni kwamba washiriki na wanajamii wanaweza kushirikishwa katika mchakato huo na kwamba ramani za jamii zinaweza kutumika kwa njia mbalimbali. Urutibu wa ramani ya mali umefanywa na vijana kutoka jamii za mijini

na vijijini, kuendelezwa na nchi zinazoendelea, na kutoka katika asili mbalimbali za kitamaduni.

Urutibu wa ramani za jamii unaweza kuwa mwanzo muhimu wa kuwashirikisha vijana na wanajamii katika mazingira mbalimbali ya kimikakati na kuchangia katika jamii zilizopangwa vyema na endelevu zaidi.

Ramani pia zinaweza kutumiwa kutambua madhara yanayoweza kutokea katika ulinzi ndani ya jamii na kuruhusu shirika kuchukua hatua za kupunguza hatari kama hizo. Iwapo watoto au vijana lazima wapitie mitaa isiyu salama ili kuja kwenye mafunzo ya michezo, jamii na polisi inaweza kushirikishwa ili kuhakikisha watoto na vijana wanaelekezwa na kulindwa wanapotembea kuelekea kwenye mafunzo.

Urutibu wa ramani unaweza pia kufanywa kwa maeneo mahususi, kama vile uwanja wa mazoezi au maeneo yatakayotembelewa wakati wa ziara ya kwenda kwenye mashindano. Kwa kutumia mchakato wa kupanga eneo kama sehemu ya Mbinu ya Kuzuia Hali inaruhusu hatari zinazohusiana na eneo kutambuliwa na kubainisha vyanzo vya usaidizi.

Urutibu wa ramani za jamii pia unaweza kutumika wakati wa kuzingatia hatari zinazohusiana na kuwa mtandaoni. Kutambua tovuti na mitandao ya kijamii ambayo inaweza kuleta madhara ya ulinzi na rasilimali zinazosaidia kuwaweka salama watoto na watu wazima walio hatarini mtandaoni

RASILIMALI

- 1. **Ulinzi wa Kimataifa kwa Watoto katika Michezo, Ulinzi wa Kimataifa kwa Watoto katika Kikundi Kazi cha Michezo, 2016,**
<https://www.sportanddev.org/en/toolkit/child-protection-and-safeguarding/international-safeguards-children-sport>
- 2. **Nyenzo za Ulinzi ya IOC,**
<https://www.olympic.org/athlete365/what-we-do/integrity/safe-sport/>
- 3. **Nyenzo za Walinzi wa FIFA,**
<https://www.fifa.com/what-we-do/fifa-guardians/#web-07>
- 4. **UEFA na Terre des hommes nyenzo za ulinzi wa mtoto kwa mpira wa miguu,** <https://uefa-safeguarding.eu/toolkit>
- 5. **Ulinzi wa Mtoto katika Rasilimali za Michezo wa NSPCC,**
<https://the cpsu.org.uk/resource-library/>
- 6. **Rasilimali za Ulinzi wa Ann Craft Trust,**
<https://www.anncrafttrust.org/resources/>
- 7. **Nyenzo za Rasilimali za Michezo kwa Maendeleo (S4D).**
<https://www.sport-for-development.com/home>



KIAMBATISHO CHA 1

FOMU YA KURIPOTI TUKIO

TAARIFA ZAKO					
Jina					
Anwani					
Nambari za mawasiliano					
Barua pepe					
Jina la shirika				Jukumu lako	

TAARIFA BINAFSI – MTOTO /VIJANA/MTU MZIMA				
Jina				Date of birth
Jinsia	Wa kiume <input type="checkbox"/>	Wa kike <input type="checkbox"/>	Si kiume wala kike <input type="checkbox"/>	Maelezo mengine (tafadhali eleza <input type="checkbox"/>
Je, kuna habari yoyote kuhusu mtoto, kijana, watu wazima walio hatarini ambayo inaweza kuwa muhimu kuzingatia?				

CONTACT INFORMATION – PARENT / CARER		
Jina		
Anwani		
Nambari za mawasiliano		
Barua pepe		
Je, wamearifiwa kutokana na tukio hili?	La <input type="checkbox"/>	Tafadhali eleza kwa nini uamuzi huu umechukuliwa
	Ndio <input type="checkbox"/>	Tafadhali toa maelezo ya kile kilichosemwa/hatua zilizokubaliwa

MAELEZO YA TUKIO*			
Tarehe na wakati wa tukio			
Tafadhali tia alama kwenye moja:	Ninaripoti wasiwasi wangu mwenyewe. <input type="checkbox"/>	Ninashughulikia masuala yaliyoibuliwa na mtu mwingine – tafadhali weka maelezo yake: <input type="checkbox"/>	
Jina la mtu aliyeibua wasiwasi		Jukumu ndani ya mchezo au uhusiano wake na mtoto/ vijana/ mtu mzima	

Nambari za mawasiliano	
Barua pepe	
Maelezo ya tukio au masuala (pamoja na taarifa nyingine muhimu, kama vile maelezo ya majeraha yoyote na kama unarekodi tukio hili kuwa ukweli, maoni, au uvumi)	

* Ambatisha na karatasi nyingine tofauti ikiwa nafasi zaidi inahitajika (kwa mfano, mashahidi wengi)

MAELEZO YA TUKIO (INAENDELEA)			
Maelezo ya Mtoto/Vijana/Walio hatarini kuhusu tukio hilo			
Tafadhali weka akaunti za mashahidi wa tukio hilo			
Jina la shahidi (na tarehe ya kuzaliwa ikiwa ni mtoto)		Jukumu ndani ya mchezo au uhusiano wake na mtoto, vijana, mtu mzima	
Anwani			
Nambari za mawasiliano			
Barua pepe			
Maelezo ya mtu yeyote aliyehusika katika tukio hili au anayedaiwa kusababisha tukio/jeraha			
Jina (na tarehe ya kuzaliwa)		Jukumu ndani ya mchezo au uhusiano wake na mtoto, vijana, mtu mzima	
Anwani			
Nambari za mawasiliano			
Barua pepe	La <input type="checkbox"/>	Ndiyo - tafadhali toa maelezo zaidi: <input type="checkbox"/>	

Jina la shirika/wakala				
Mtu wa Kuwasiliana naye				
Nambari za mawasiliano				
Barua pepe				
Hatua iliyokubaliwa au ushauri uliotolewa:				

AZIMIO					
Saini yako					
Andika jina					
Tarehe ya Leo					

Wasiliana na Afisa Mteule wa Ulinzi wa shirika lako kwa mujibu wa [weka jina la shirika lako] taratibu za kuripoti					
Jina la Afisa Mteule wa Mlinzi					
Tarehe iliyoripotiwa					

* Imetolewa kutoka kwa Fomu ya Kuripoti Matukio ya Kitengo cha Ulinzi wa Mtoto NSPCC

DOWNLOAD 

<https://www.sport-for-development.com/imglib/downloads/safeguarding/giz-2021-en-incident-reporting-form-safeguarding-in-sport-and-s4d-contexts.docx>

KIAMBATISHO CHA 2

FOMU YA IDHINI YA UPIGAJI PICHA NA FILAMU

Kwa mujibu wa sera yetu ya ulinzi, hatutaruhusu picha, video au picha nyingine za watoto, vijana, au watu wazima walio hatarini kupigwa bila idhini. Iwapo mtoto yuko chini ya miaka 16, ni lazima idhini ipatikane kutoka kwa mzazi/mlezi.

(Ikiwa mtoto ana umri wa zaidi ya miaka 16, ni desturi nzuri kuwajulisha wazazi/walezi kwamba picha na/au video za mtoto wao zinaweza kutumika ikiwa mtoto ametoa idhini.)

Idhini lazima itolewe kutoka kwa walezi ambapo mtu mzima yuko chini ya uangalizi na hawezi kutoa kibali.

[Jina au klabu au shirika] itachukua hatua zote ili kuhakikisha kuwa picha hizi zinatumika kwa madhumuni yaliyokusudiwa.

Ukifahamu kuwa picha hizi zinatumika vibaya, tafadhali tujulishe mara moja.

Jina la mtoto, kijana au mtu mzima		Umri	
---	--	-------------	--

Azimio la idhini - mtoto mwenye umri wa miaka 16 au zaidi

Tafadhali weka alama kwa kila kijisanduku (au toa kile usichokubali), kisha utie saini kwenye fomu hii.

<input type="checkbox"/>	Ninatoa ruhusa ya picha yangu kutumika ndani ya kilabu kwa madhumuni ya maonesho.		
<input type="checkbox"/>	Ninatoa ruhusa ya picha yangu kutumika ndani ya machapisho mengine yaliyochapishwa.		
<input type="checkbox"/>	Ninatoa ruhusa ya picha yangu kutumika kwenye tovuti ya klabu.		
<input type="checkbox"/>	Ninatoa ruhusa ya picha yangu kutumika kwenye kurasa za mitandao ya kijamii za kilabu.		
<input type="checkbox"/>	Ninatoa ruhusa ya video yangu kutumika kwenye tovuti ya klabu.		
<input type="checkbox"/>	Ninatoa ruhusa ya video yangu kutumika kwenye kurasa za mitandao ya kijamii za kilabu.		
<input type="checkbox"/>	Ninatoa ruhusa ya video yangu kutumika kwa madhumuni ya mafunzo au uchanganuzi.		
Saini		Tarehe ya Leo	

AZIMIO LA IDHINI – MZAZI/MLEZI WA MTOTO CHINI YA MIAKA 16 AU MTU MZIMA CHINI YA UANGALIZI

Tafadhali weka alama kwa kila kijisanduku (au toa kile usichokubali), kisha utie saini kwenye fomu hii.

<input type="checkbox"/>	Ninatoa ruhusa ya picha ya mtoto wangu au mtu mzima aliye katika uangalizi itumike ndani ya klabu kwa madhumuni ya maenesho.
<input type="checkbox"/>	Ninatoa ruhusa ya picha ya mtoto wangu au mtu mzima aliye chini ya uangalizi itumike ndani ya machapisho mengine yaliyochapishwa.
<input type="checkbox"/>	Ninatoa ruhusa ya picha ya mtoto wangu au mtu mzima aliye chini ya uangalizi itumike kwenye tovuti ya klabu.
<input type="checkbox"/>	Ninatoa ruhusa ya picha ya mtoto wangu au mtu mzima aliye chini ya uangalizi itumike kwenye kurasa za mitandao ya kijamii za klabu.
<input type="checkbox"/>	Ninatoa ruhusa ya picha ya mtoto wangu au mtu mzima aliye chini ya uangalizi itumike kwenye tovuti ya klabu.
<input type="checkbox"/>	Ninatoa ruhusa ya picha ya mtoto wangu au mtu mzima aliye chini ya uangalizi itumike kwenye kurasa za mitandao ya kijamii za klabu.
<input type="checkbox"/>	Ninatoa ruhusa kwa video ya mtoto wangu au mtu mzima aliye chini ya uangalizi itumike kwa madhumuni ya mafunzo au uchanganuzi.
<input type="checkbox"/>	Ninathibitisha kwamba nimesoma, au nimefahamishwa, jinsi picha au video hizi zitakavyohifadhiwa ndani ya shirika.
Saini	Tarehe ya Leo
Andika jina	

* Imechukuliwa kutoka Fomu ya Idhini ya Ulinzi wa Mtoto ya NSPCC katika Kitengo cha Matukio cha Upigaji Picha na Kurekodi Filamu

[DOWNLOAD !\[\]\(a03a7eb2f4046e1d3c76772003e549ea_img.jpg\)](https://www.sport-for-development.com/imglib/downloads/safeguarding/giz-2021-en-photography-and-filming-consent-form-safeguarding-in-sport-and-s4d-contexts-.docx)
<https://www.sport-for-development.com/imglib/downloads/safeguarding/giz-2021-en-photography-and-filming-consent-form-safeguarding-in-sport-and-s4d-contexts-.docx>

